

ARUSI YA MWANA-KONDOO



Asante, Ndugu Edward. Bwana akubariki.

Habari za jioni marafiki. Hakika ni majaliwa tena usiku wa leo kuwa hapa kwenye Maskani ya Ushirika. Nilipopitia hapa, alasiri ya leo, na kuangalia mahali ilipokuwa, na nikaona neno “Ushirika,” hilo lilinifaa vizuri kabisa. Ninapenda hilo, Ndugu Edward. Ushirika, huo ndio tunaoamini.

² Rafiki yangu wa siku nyingi, ambaye ndio kwanza aende Nyumbani kuwa pamoja na Bwana, wengi wenu huenda mlimjua, Dkt. F. F. Bosworth. Wengi wenu. Alikuwa hapa Phoenix, ninaamini, pamoja nami wakati mmoja, mtu hodari sana. Naye alikuwa ninii... alikuwa na—na... Alikuwa mzee mtakatifu, lakini alikuwa na ucheshi. Naye aliniambia, wakati mmoja, alisema... Nilifululiza kuzungumza juu ya ushirika. Naye akasema, “Ndugu Branham, unajua ushirika ni nini?”

Nikasema, “Vema, nafikiri ninajua, Ndugu Bosworth.”

³ Akasema, “Ni jamaa wawili katika meli moja.” Kwa hiyo, na hivyo ndivyo karibu ulivyo, kushiriki chumba kimoja mmoja kwa mwingine.

⁴ Nami niliona wengi wenu mmeinua mikono yenu, mnaomjua Ndugu Bosworth. Kwa kuwa kwamba—kwamba mlimjua, ningetaka kusema neno la wakati wake wa mwisho hapa duniani. Nilikuwa nimemjua kwa muda fulani. Naye alikuwa akienda huko uwanjani akihubiri Injili na kuwaombea wagonjwa, kabla sijazaliwa. Kwa hiyo mnaweza kuona alikuwa kwenye umri gani. Bwana alimjalila kuishi, nafikiri, karibu miaka themanini na mitano, kitu kama hicho, na angali alikuwa ni mzee shujaa wakati alipokufa.

⁵ Wakati alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, naamini ndivyo alikuwa, mimi na yeye tulikuwa kwenye... ninaamini, Hoteli ya Edgemont huko Miami. Nasi tulikuwa tumekwisha kula chakula che—chetu cha jioni, na tukatoka tukaenda pwani ambako mawimbi yalikuwa yakiingia, kuangalia mwezi ukipanda. Nami huyu hapa, yapata umri wa miaka arobaini, mabega yangu yameinama chini, nikitembea namna hiyo. Naye, yapata umri wa miaka sabini na mitano, amenyooka wima tu jinsi angaliweza kuwa. Nami nikamwangalia, na nikampenda. Ndipo nikasema, “Ndugu Bosworth, ninataka kukuuliza swali.”

Akasema, “Endelea tu, Ndugu Branham.”

Nami nikasema, “Ni lini ulipokuwa kwenye wakati wako mzuri kabisa?”

⁶ Akasema, “Sasa hivi.” Vema, basi, nilijisikia kuaibika. Pia akasema, “Unasahau ya kwamba mimi ni mtoto mdogo tu, nikiishi katika nyumba iliyochakaa,” akasema. Na huyo alikuwa ni Ndugu Bosworth.

⁷ Niliposikia ya kwamba alikuwa akienda kukutana na Bwana, Karibu niunguze tairi kutoka kwenye gari langu, nikishuka kwenda Miami, nikamwone. Ndipo wakati mimi na mke wangu tulipofika kule... Na familia ya Bosworth na familia yetu tulikuwa marafiki wakubwa. Basi tukaingia. Huyo mzee mheshimiwa amelala kwenye kitanda kidogo. Naye alikuwa ameinuka, maskini kichwa chake chenye upara, ameninyoshea mikono midogo, myembamba, namna *hiyo*. Machozi yakitiririka mashavuni mwangu. Nilimkumbatia kwa mikono yangu, nikasema kwa sauti kuu, “Baba yangu, baba yangu, magari ya Israeli na wapanda farasi wake!” Kwa sababu, kama kulipata kuwako na mzee ambaye aliweka heshima katika uamsho wa Kipentekoste, ilikuwa ni Ndugu Bosworth. Hakika alikuwa hivyo. Alikuwa ua kuu.

⁸ Nanyi mwajua, jambo la kwanza analotaka kufanya, ni kuniambia kichekesho kidogo, namna hiyo, mwajua.

Nami nikasema, “Ndugu Bosworth, je! utapona?”

⁹ Akasema, “La, Ndugu Branham. Mimi si mgonjwa, kwanza.” Akasema, “Ninaenda tu Nyumbani.”

Nikasema, “Vema, hilo ni sawa kabisa.”

¹⁰ Tulikuwa tu ndio kwanza tutoke hudumani huko Afrika, yeye na mimi. Akasema, “Mimi ni mzee sana kuishi zaidi.” Akasema, “Ninaenda Nyumbani.”

Nikasema, “Ndugu Bosworth, ungenishauri nifanye nini?”

¹¹ Naye akasema, “Dumu na Injili.” Kisha akasema, “Rudi kwenye huduma ya umishenari upesi uwezavyo.” Kasema, “Huo ungekuwa ndio ushauri wangu.”

¹² Nami nikasema, “Ndugu Bosworth, jambo moja zaidi ningetaka kukuuliza.”

Akasema, “Ni lipi, Ndugu Branham?”

¹³ Nikasema, “Sasa, umemtumikia Bwana karibu miaka sitini, katika huduma, ama labda zaidi.” Kisha nikasema, “Wakati wako wa furaha sana maishani ulikuwa ni upi?”

Akasema, “Sasa hivi.”

Nami nikasema, “Ndugu Bosworth, unajua unakufa?”

¹⁴ Akasema, “Siwezi kufa. Nilikufa miaka mingi iliyopita.” Nami... Akasema, “Ndugu Branham, yote niliyopenda na kuyajali kwa miaka sitini iliyopita, ninamngojea Yeye aufungue mlango ule wakati wowote na aje, akanichukue.”

Ninawazia jambo hilo, *Zaburi Ya Maisha*.

Maisha ya watu mashuhuri yote
 yanatukumbusha
 Tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
 Tunapoachana, tunaacha nyuma yetu
 Nyayo za miguu katika mchanga wa wakati.

Na hakika yeye aliacha nyayo za miguu, kwangu mimi.

¹⁵ Kabla hajafa, ama kua- . . . kuingia Utukufuni, yapata saa moja, ama labda zaidi, kabla hajaaga dunia. Kwa namna fulani alikuwa amelala kwa muda wa saa chache; na mke wake, wanawe, wapendwa wake wamesimama karibu naye, ndipo mzee huyo akaamka, akaangalia kote, akasimama, na kukimbia sakafuni, na akapeana mikono na mama yake ambaye alikuwa ameaga dunia kwa miaka mingi, pamoja na baba yake. Na kwa zaidi ya saa moja, alipeana mikono na watu, akisema, “Huyu ni Ndugu John. Naam, ulikuja kwa Kristo katika mkutano wangu huko Joliet, Illinois. Huyu hapa Ndugu . . .” Akipeana mikono na waongofu wake waliokuwa wameaga dunia, wameondoka kwa muda wa miaka mingi.

¹⁶ Na—nawaambia, wakati mwingine ninaamini ya kwamba katika hiyo saa tunayopita kutoka dunia hii kuingia nyingine, ninaamini wakati fulani wakati . . . Ule mto utakuwa mgumu kuvuka, kwa vyovyote vile, unajua. Ninaamini labda Bwana huwaambia wapendwa wetu, “Shukeni mwende mtoni mkawalaki kule chini.” Kwa kuwa kama Yakobo alivyosema, tutakusanyika pamoja na watu wetu siku moja.

¹⁷ Mimi pia ninaitazamia siku hiyo kuja. Na halafu wakati nitakapomaliza na maisha haya hapa, ama Mungu atakapomaliza nami hapa, na nione ya kwamba nimeteka kila ngome niliyoweza, nikapitia katika kila kiwanja cha miiba, na kupanda kila kilima, ninataka kuangalia nyuma, nione mahali ambapo nimekuwa, nitakapofika mtoni.

¹⁸ Daima nimesema, kama jamaa weusi hapa, wana maskini wimbo mdogo wanaoimba, “Sitaki shida yoyote pale mtoni.” Ninataka kunyosha yote sasa.

¹⁹ Labda tu nirudishe upanga kwenye ala, na nivue helmeti, na kuiweka chini ufukoni, na kuinua mikono yangu, na kupiga kelele, “Lete mashuaokozi, Baba. Ninakuja nyumbani asubuhi hii.” Yeye atakuwepo pale. Usifadhaike. Ninaamini jambo hilo. Nafikiri hiyo ndiyo shauku ya kila mmoja wa mioyo yetu.

²⁰ Sasa, kweli ni majaliwa makuu kuwa hapa usiku wa leo pamoja na mchungaji huyu mzuri sana na kanisa lake, na kazi hii nzuri sana, na hawa wageni katika Kristo, katika upande huu wa Phoenix. Kwa kuwa, hakika, sisi ni wageni. Sisi ni wasafiri na wageni hapa. Tunautafuta Mji.

²¹ Kama nilivyokuwa nikihubiri asubuhi ya leo kwenye maskani ya Ndugu Fuller, juu ya Uzao wa Kifalme. Sasa, kama mna vinasasauti, mimi huwa sitaji. Lakini kuna jambo

fulani lililotukia asubuhi ya leo, ambalo mimi...Kama una kinasasauti, kama ukipata moja ya hizo kanda, nina hakika utaifurahia. Ndugu Maguire anazo, na *Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu*.

²² Unaona, Uzao wa Ibrahimu ulikuwa ni Isaka, ambaye ni wa Kiyahudi, kimwili. Lakini Uzao wa Kifalme ulikuwa ni Kristo, kupitia ile ahadi, na huyo Kristo alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Na limo moyoni mwetu leo tunaponinii... “Kama Mimi...Ninyi mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu, basi ombeni mtakalo, nanyi mtatendewa.”

²³ Sasa, nilielezea jambo hilo, kuhusu Phoenix, mara nyingi tangu nimekuwa hapa...Mara yangu ya kwanza kuja ilikuwa ni miaka thelathini na mitano iliyopita. Na huko kwenye mtaa wa 16 na Henshaw, nilikoishi, nikafanya kazi kwenye Ranchi ya Duara R huku, kutoka Wickenburg. Nami nilienda pamoja na msichana mdogo kule kwenye mtaa wa 16 na Henshaw. Nilienda kupatafuta mahali pale hivi majuzi, na hata si Henshaw tena. Ni Buckeye sasa. Na ni jiji kubwa moja kwa moja katika eneo la mji mkuu wa Phoenix hapa. Kila kitu kimebadilika sana.

²⁴ Ndipo mke wangu na mimi tulipanda tukaenda kwenye Mlima wa Kusini, kuutazama Phoenix. Nikawaza, yapata miaka mia tatu iliyopita, labda hakukuwako na kitu hapa ila mbwa mwitu, mipungate, na kadhalika. Na sasa ni jiji kubwa la ajabu. Sasa, nikasema, “Mpenzi, umeongoka ama umepotoka? Unaweza kutumia chaguo lako. Kwangu mimi, umepotoka sasa. Kwa sababu, majengo haya makubwa na majengo mazuri ingekuwa ni sawa kama wanaume na wanawake walikuwa wakitembea huku na huko mitaani, wamemwinulia Mungu mikono yao juu, wakimsifu Mungu, na ndugu na dada wakiishi hivyo; badala ya kunywa pombe, kucheza kamari, kuvuta sigara, kusema uongo, kuiba, vilabu vya pombe, kila kitu ambacho ni kiovu. Katikati ya hayo yote, ingawaje...”

Ndipo mke wangu akaniambia, “Basi, Billy, uko hapa kwa sababu gani?”

²⁵ Nikasema, “Lakini, mpenzi, tangu tulipoketi hapa, dakika kumi na tano, ni mara ngapi uongo umesemwa kote katika bonde lile? Ni viapo vingapi vimeapwa, Jina la Bwana bure? Ni sigara ngapi, unywaji kiasi gani wa viski, ni matendo mangapi ya uzinzi yamefanywa, na kote kupitia kule, katika tu muda mfupi uliopita, tukiwa hapa?”

Akasema, “Hilo si ni jambo baya sana?”

²⁶ Lakini nikasema, “Hii hapa sababu ya sisi kuwa hapa, mpenzi. Ni maombi mangapi ya uaminifu yamepaa juu tangu tumekuwa hapa? ‘Ninyi ni Nuru ya ulimwengu.’ Hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa hapa, kutia shime pamoja na makanisa haya madogo hapa, kufanya kila tuwezalo, kulisaidia jambo hilo liendelee. Kuwa ninii...”

²⁷ Ninyi nyote, ninyi watakatifu, ni baraka kwangu. Ninatumaini ya kwamba nitakuwa baraka kwenu, katika kuwatembelea hapa. Nami, nilipoona kwamba nitayatembelea madhehebu mbalimbali na mashirika, na—na makanisa mbalimbali, na kadhalika, ndugu hawa kote katika bonde hili la Phoenix hapa, moyo wangu ulifurahi sana. Hilo linakuja kabla ya ule mkutano nitakaohubiria, kwenye mkutano wa Wafanyabiashara Wakristo mnamo, nafikiri, kiamshakinywa cha Jumamosi asubuhi, na halafu mkutano wa Jumapili alasiri, utakaofuata, Jumapili hiyo ifuatayo. Na daima ni majaliwa kukutana na ndugu hao. Nafikiri wana karibu viti elfu mbili na mia tano kule. Kutakuwa na nafasi kubwa ya kuketi kwetu sisi sote. Nasi tunatarajia kukutana nanyi kule.

²⁸ Na halafu kuwa na wakati huu wa ushirika, kwenda kutoka kanisa moja hadi lingine, na kuhubiri. Nafikiri nilihubiri asubuhi ya leo mpaka nikapwelewa na sauti, kwa yapata saa moja na nusu. Na huo ulikuwa ni mfupi. Kwa kawaida sitoki kabla ya saa tatu ama nne za huo, hu—huko kwenye kanisa la nyumbani. Ninaninii tu. . . Mimi si mhubiri. Kwa hiyo ni—ninafanya tu kelele za shangwe kwa Bwana. Ninapenda kufanya hivyo vizuri sana. Na—nadhani ninapenda tu jambo hilo, kwa hiyo ninaendelea tu kulifanya. Nimekuwa na matamshi manne ama matano mbalimbali, ninawachelewesha watu sana, kwa hiyo ninajua hiyo ni kweli. Na usiku wa leo, kusema kweli, tutakuwa tumetoka hapa kabla ya saa saba. Mimi, karibu tu nitawahakikishia jambo hilo. Ninaninii tu, karibu. . . Hisi nzuri sana ya roho, na kila kitu ni kizuri sana, nina hakika Roho Mtakatifu atakuwa na baraka kwetu.

²⁹ Sasa, sasa sijakuwa na ibada zozote za uponyaji katika mikutano hii. Mimi. . . Usiku mmoja, huko chini kwa ndugu. . . Jina la Yesu, huyo mchungaji alikuwa ni nani? Ndugu Outlaw. Kanisa la Ndugu Outlaw, kulikuwako na wengi sana kule waliotaka kuombewa. Nami nikamwagiza mwanangu asambaze kadi kadhaa za maombi. Na halafu siku chache usiku, Roho Mtakatifu akishuka sana kwenye jengo hilo, mpaka. . . Nyote mnajua. Mmekuwa kwenye mikutano yangu. Nyote mmekuwako. Mmeona jinsi utambuzi, na kadhalika. Lakini sasa nimeona inawakusanya wengi wa kuombewa. Na niliona ya kwamba wa kwanza, kwa kuanzia Jumatano na Alhamisi. Nilifikiri ningengojea mpaka baada ya Jumapili, kwa sababu kama mnafanya ibada za uponyaji kanisani. . .

³⁰ Unaona, ni—nilitangaza kila nilikokwenda kwamba kila mtu akae kwenye wajibu wake Jumapili, unaona. Mikutano hii maalumu ni kuwatembelea tu ndugu. Na tu—tunataka kila mtu kukaa kwenye wajibu wenu, maana mchungaji wenu anawangojea, na huko ndiko unakopaswa kuwa.

³¹ Kwa hiyo basi—basi nafikiri, kesho usiku, Bwana akipenda, sininii. . . Tutakuwa wapi kesho usiku? [Ndugu mmoja anasema,

“Huko Tempe, kwenye kanisa la Ndugu O'Donnell.”—Mh.] Ndugu O'Donnell, huko Tempe, Arizona. Sasa, kama hamna jambo lo—lolote maalum linaloendelea kanisani mwenu, na mna wagonjwa, mbona, nitawaombea wagonjwa, kesho usiku, kufanya tu mstari wa kawaida wa maombi, kuwaombea wagonjwa, labda—labda Jumatatu, Jumanne. Hebu tuone, ninapaswa... Sijui. Je! nina ibada Jumatano usiku pia? [“Ndiyo.”] Jumatano usiku. Basi itaninii... .

³² Na unaanza Alhamisi, siyoy, mkutano huo? [Ndugu mmoja anasema, “Kwa namna fulani nilininii mambo...?... mkutano.”—Mh.] Vema, ndugu. Atatangaza sasa. [“Mnaona, tuko hapa usiku wa leo. Na kesho usiku tuko kwenye Assembly of God huko Tempe. Na halafu Mountain View, huko Sunnyslope tarehe ishirini na tatu. Na halafu kwenye Central Assembly tarehe ishirini na nne.”] Vema, hilo ni sawa. [“Nisingeweza kukumbuka, mimi mwenyewe. Kwa namna fulani nilichanganyikiwa na jambo hilo.”] Usifikirie jambo hilo.

Nilikuwa nikizungumza hivi majuzi, kuhusu, “Nisingeweza kukumbuka.”

³³ Naye Ndugu Jack Moore aliniambia, akasema, “Unafikiri wewe hali yako ni mbaya?” akasema.

³⁴ Nikasema, “Ndugu Jack, nikianza kuzungumza, siwezi kukumbuka kamwe yale niliyokuwa nikizungumzia.”

³⁵ Akasema, “Usifikiri hiyo ni hali mbaya.” Kasema, “Ninapiga simu, ninampigia mtu fulani, nasema, ‘Unataka nini?’” Vema, hali hiyo inakuwa mbaya sana!...?... Loo!

³⁶ Kwa hiyo, jamani, hilo linaweza likasikika la kichekesho, jambo ambalo sidhani ni sawa kusema mimbarani hapa. Lakini watoto wa Mungu ni watoto tu wenye furaha, kwa vyovyote vile, mwajua, kwa hiyo tu—tunapenda tu kufanya hivyo. Nilifikiri hilo kwa namna fulani lilikuwa ni zuri.

³⁷ Ninyi nyote, wengi wenu, mnamjua Ndugu Jack Moore. Yeye anatoka Shreveport, Louisiana, Maskani ya Uzima, ndugu mzuri sana. Na kwa hiyo alikuwa akiniambia jambo hilo. Yeye ni kontrakta, pia.

³⁸ Alisema, “Usifikiri hiyo ni hali mbaya, Ndugu Branham.” Kasema, “Nilimpigia simu mtu fulani hivi majuzi, nikapiga namba zao.” Kisha akasema, “Walijibu, kasema, ‘Haloo.’ Nikasema, ‘Vema, unataka nini?’”

Nikawazia, “Vema, hilo linafikia kule chini kabisa, Ndugu Jack.”

³⁹ Kwa hiyo sasa, nafikiri lingekuwa ni jambo jema, na hawa marafiki wanaotaka kuombewa, na kuwaleta wagonjwa wao, basi tutawaombea.

⁴⁰ Sasa, usiku wa leo, nimewazia juu ya yale ningesema usiku wa leo hapa katika maskini kanisa hili zuri. Niliwazia,

“Vema, sijui kitu gani.” Inanibidi tu kuchukua tu somo dogo, na kutumainia kwamba Bwana atayachanganya maneno hayo mahali fulani, na kuyaacha yaangukie mahali ambapo yatamsaidia mtu fulani. Kuwa... Kamwe sijaribu kuchukua somo. Daima ninajaribu kujisikia kuongozwa, na kuandika Maandiko kadhaa, na kadhalika. Na—na halafu, kama Bwana akiongoza vinginevyo, basi ninaenda tu jinsi anavyoongoza. Nami ninafikiri hivyo ndivyo sote tunavyopaswa kufanya. Sivyo? Kufanya vivyo hivyo.

⁴¹ Na sasa kuna jambo moja ambalo—ambalo na—nataka, kila mmoja wa kanisa atangaze jambo hili kwa kila kundi la mahali hapo. Na hiyo ni, kwamba endapo... Mtakapomaliza kumwombea mchungaji wenu na wapendwa wenu, msinisahau, maana ninatambua, kila siku, zaidi ya hapo awali, ya kwamba tunaelekea kwenye mwisho wa safari.

⁴² Na ndiyo kwanza nimzike mama yangu, majuma machache yaliyopita. Nami nilimshika mikononi mwangu mpaka Mungu alipochukua pumzi yake na nafsi yake Mbinguni. Nilitazama hayo mauti ya kishujaa ya mwanamke aliyejazwa na Roho Mtakatifu, na nikamwona akija moja kwa moja kwenye mwisho wa safari. Niliwazia, “Loo, si—sina budi kumfanya kila mama namna hiyo. Lazima tu nifanye jambo fulani kuninii... kufanya niwezalo, kuwafanya watu waone kweli linamaanisha nini.”

⁴³ Na, enyi marafiki, nimeshawishika ya kwamba labda lina kilindi kidogo. Nami nafikiri tunalichukua kidogo kwa wepesi kupita kiasi kuliko vile lilivyo hasa. Nafikiri ya kwamba inatupasa kukumbuka. Kama Mungu ni mtakatifu sana hata Malaika wanaonekana wachafu mbele zake, sisi nasi tunaonekanaje? Unaona? Hiyo ni kweli. Kwa hiyo tunahitaji kukumbuka. Pia kumbukeni, Mungu ameketi huko mbali katika Umilele, anayewaka kuliko majua yote katika mfumo wa juu. “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu,” Malaika wakiwa na mbawa juu ya nyuso zao, na juu ya miguu yao, wakiruka katika Uwepo Wake, wakilia, “Mtakatifu.” Tunapaswa kuwa nini? Kwa hiyo sisi... Hivyo ndivyo tunavyojaribu kufanya.

⁴⁴ Na—najisikia namna hiyo huu, Ufalme wa Mungu, ni kama mtu aliyechukua jarife akaenda baharini, Yesu alisema, naye akalitupa ndani. Na wakati alipolivuta, alichukua za aina nyingi. Lakini samaki wazuri, bila shaka, waliwekwa; na hao samaki wengine wala mizoga walirudi majini, kama vile kamba wa maji baridi, na—na nyoka, mijusi, na kasa, na kadhalika. Lakini majarife ya Injili huwashika wote. Nasi tunaninii... Kutakuwako na siku ambapo tutatupa jarife letu la mwisho, Ndugu Adams. Hilo ni kweli. Si juu yako ama mimi kusema yupi ni samaki na yupi si samaki. Hatujui. Tunatupa tu jarife na kulivuta. Hivyo tu. Mungu anawajua walio Wake. “Wale aliotangulia kuwajua, Yeye aliwaita; na wale aliwaita, amewahesabia haki; na wale ambao amewahesabia

haki, amewatukuza.” Kwa hiyo tunangojea, tunatupa tu jarife. Na ni majaliwa yangu usiku wa leo kusimama katika kanisa la Ndugu Edward hapa kusaidia kutupa jarife mahali hapa, kuona kama kuna samaki yeyote ambaye Mungu anaye kwa ajili ya Ufalme Wake.

⁴⁵ Sasa, kabla tu hatujasoma Neno, na tuzungumze na Mwandishi wa Neno kidogo tu tunapoinamisha vichwa vyetu.

⁴⁶ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, katika utakatifu wa wakati huu, ambao tunalikaribia Neno la Mungu aliye hai, ambalo ni Mungu, sijui kama kungekuwako na watu wowote hapa ndani walio na haja mioyoni mwao, ambao wangetaka kukumbukwa katika maombi haya. Fanya ijulikane kwa kuinua mkono.

Bwana Yesu, angalia wasikilizaji hawa, kwa kuwa unajua kila moyo.

Asante.

⁴⁷ Mungu mwenye rehema sana na mtakatifu, Mwenyezi, El Shaddai, ambaye alimtokea Ibrahimu katika Jina la “Mwenyezi, Mungu mwenye maziwa, Mpaji nguvu, Mwenye kuwalisha wanyonge,” tujie usiku wa leo, Baba. Nasi tunatambua unyonge wetu na makosa yetu. Tunakiri dhambi zetu mbele Zako, na kuziweka kwenye madhabahu Yako ya shaba ya hukumu, na kuomba ya kwamba Damu ya Yesu Kristo iziondolee mbali, katika sadaka tunayotoa. Tujalie hilo, Ee Mungu.

⁴⁸ Tunayatoa maisha yetu na yote tuliyo nayo, na talanta ndogo tuliyo pewa. Bwana, itumie kwa utukufu wa Mungu.

⁴⁹ Bariiki kanisa hili, mchungaji wake mzuri, mashemasi, wadhamini, na halmashauri yote, na kila mshiriki anayeingia katika kanisa hili linaloitwa “Ushirika.” Mungu, ninaomba ya kwamba wanaume na wanawake, wanapoingia kwenye mlango ule wa mahali hapa, kwamba wataanguka chini ya ushawishi kwa sababu ya utaratibu mzuri sana wa Roho Mtakatifu ndani ya jengo hili. Tujalie hayo, Bwana.

⁵⁰ Samehe dhambi zetu, na makosa yetu, tunaomba tena. Wakumbuke wale walioinua mikono yao. Chini ya mkono huo, Bwana, kulikuwa na moyo uliohitaji jambo fulani kutoka Kwako, na labda Wewe peke Yako Ndiwe unayeweza kuwapa. Naomba ya kwamba utawajalia, Baba. Chochote wanachohitaji, wape kwa wingi. Kukiwako na mgonjwa yeyote, Bwana, waponye. Kukiwako na yeyote anayeanguka kando ya njia, mtie nguvu huyo, goti hilo nyonge. “Mwanzi uliopondeka, hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima.” Nasi tunajua ya kwamba kamwe hatakataa mwanzi uliopondeka; Yeye ataurekebisha. Nami ninaomba, Baba wa Mbinguni, kama kuna roho zenye huzuni, ama—ama kuvunjwa moyo, ama mikono minyonge inayoning’inia chini, na magoti yaliyolegea, jalia wainuliwe usiku wa leo, Bwana. Jalia Roho Mtakatifu aje na

kuiponya mioyo na roho zetu, na miili yetu, nasi tutampa sifa zote kwa ajili ya jambo hilo. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

⁵¹ Kama mngpenda kuyageukia Maandiko, kwa mahubiri ya karibu dakika thelathini tu, ningetaka msome pamoja nami kutoka katika kitabu cha Ufunuo, mlango wa 19. Na ningetaka kusoma kufikia kifungu cha 7, vyote pamoja.

Baada ya hayo nikasikia sauti kama sauti ya makutano mengi, sauti kubwa mbinguni, ikisema, Haleluya; Wokovu, . . . utukufu, na heshima, na nguvu, zina Bwana Mungu wetu;

Kwa kuwa hukumu zake ni za kweli na za haki; maana amemhukumu yule kahaba mkuu aliyeiharibu nchi kwa uasherati wake, na kuipatiliza damu ya watumwa wake mkononi mwake.

Wakasema mara ya pili, Haleluya. Na moshi wake hupaa juu hata milele na milele.

Na wale wazee ishirini na wanne, na wale wenye uhai wanne, wakasujudu na kumwabudu Mungu, aketiye katika kile kiti cha enzi, wakisema, Amina, Haleluya.

Sauti ikatoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Msifuni Mungu wetu, enyi watumwa wake wote, ninji mnaomcha, wadogo kwa wakuu.

Nikasikia sauti kama sauti ya makutano mengi, na kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi yenye nguvu, ikisema, Haleluya; kwa kuwa Bwana Mungu wetu, Mwenyezi, amemiliki.

Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejweka tayari.

⁵² Ningetaka kuzungumza usiku wa leo juu ya somo la: *Arusi Ya Mwana-Kondoo*, kwa dakika chache tu kuninii . . . Tunalifahamu sana Andiko hili. Hapana shaka ila mchungaji wenu mzuri hapa ameliendea somo hili mara nyingi.

⁵³ Na, hilo, tunajua ya kwamba kutakuwa na Bibi-arusi, na kutakuwa na karamu ya arusi itakayoandaliwa mbinguni. Hiyo itakuwako hakika, kama Mungu alivyo, kwa sababu ni Neno Lake. Nasi tunajua ya kwamba wale watakaofanyiza Bibi-arusi huyo watakuwa ndio Kanisa Lake, nao wataonekana mbele Zake bila waa wala kunyanzi. Nao wana nyenzo duniani sasa za kujifanya tayari. Kama ukiangalia, Hilo lilisema, "Amejifanya tayari."

⁵⁴ Wengi sana husema, "Kama Mungu atamwondoa roho huyu mchafu kutoka kwangu, kuacha kunywa pombe, ama kuacha kucheza kamari, ama kusema uongo, ama kuiba, nitamtumikia."

⁵⁵ Lakini hilo ni juu yako. Unaona, inakupasa kufanya jambo fulani, pia. “Wale washindao watarithi vitu vyote.” Wale washindao. Una nguvu za kufanya hivyo, bali inakupasa kuwa tayari kuiweka chini. Unaona?” “Amejifanya tayari.” Ninapenda Neno hilo.

⁵⁶ Unaona, Mungu asingeweza kutusukuma kupita kwenye bomba dogo, atuvute atutoe upande wa pili, halafu aseme, “Heri yeye ashindaye.” Hukuwa na jambo lolote la kushinda; Yeye alikusukuma tu ukapita. Lakini inakubidi kujiamulia mambo mwenyewe. Inanibidi kujiamulia mambo mwenyewe. Katika kufanya jambo hilo, tunaonyesha imani na heshima zetu kwa Mungu.

⁵⁷ Ibrahimu aliahidiwa mwana, lakini hana budi kudumisha ahadi hii kwa muda wa miaka ishirini na mitano, heri na shari alizokuwa nazo, na majaribu, katika miaka hiyo ishirini na mitano. Lakini yeye alishikilia neno hilo la ahadi.

⁵⁸ Nao Israeli waliahidiwa nchi ya ahadi, bali iliwabidi kupigania kila inchi yake. “Kila mahali nyayo za miguu yenu zitakapokanyaga, hapo nimewapa ninyi,” Mungu alimwambia Yoshua. Yote ilikuwa pale. Nchi ilikuwako, naye Mungu aliwapa hiyo, bali hawana budi kuipigania.

⁵⁹ Ndivyo ilivyo kuhusu uponyaji wa Kiungu. Mungu ana nguvu za kukuponya, kama una ujasiri wa kuukubali, bali utapigania kila inchi ya njia hiyo.

⁶⁰ Mungu ana neema ya ajabu ya kukuokoa, Naye atafanya hivyo, bali utapigania kila inchi ya njia yako.

⁶¹ Nimekuwa nyuma ya mimbara, nikiendelea kwa muda wa miaka thelathini na moja, na kila inchi ya hiyo imekuwa ni vita, daima. Hakika imekuwa ni vita.

⁶² “Lakini hatuna budi kupigana kama inatubidi kutawala.” Kwa hiyo tunakuta ya kwamba inambidi Bibi-arusi kujifanya tayari Mwenyewe. “Tuwe tayari kuweka kando kila mzigo utuzingio kwa upesi, tupate kupiga mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele zetu.” Hatuna budi kuiweka kando, sisi wenyewe. Hatuwezi kusema, “Mungu, Wewe njoo, iweke kando kwa ajili yetu.” Inatupasa kufanya hivyo, sisi wenyewe.

⁶³ Sasa, ninapenda kuwazia juu ya arusi. Nimekuwa na majaliwa ya kuwafungisha ndoa watu kadhaa. Nami nafikiri, ninapomleta kijana mwanamume na kijana mwanamke madhabahuni, na kuwaona wakishuka kupitia kanisani; naye msichana, mrembo akiwa amevaa nguo zake za arusi, na utaji juu ya uso wake na ukining’inia chini; na bwana arusi, amenyooka wima, amevaa nadhifu; na ni kijana na amejaa nguvu, wanaposhuka kwenda kule katika ubora kabisa wa maisha yao, na kuweka nadhiri hiyo ya ndoa, nafikiri kuna jambo tamu kulihusu. Kuna kitu fulani kitakatifu, kwa sababu

inanikumbusha ya kwamba kutakuwako na arusi nyingine kuu siku moja, wakati bibi-arusi wa Kristo atakapokuja akitembea kwenye vishoroba vya Utukufu.

⁶⁴ Bwana-arusi atakuwa na kila kitu tayari. Kutakuwako na arusi na chakula cha jioni. Jinsi tunavyopenda kuwazia juu ya kuketi mezani tukiangaliana sisi kwa sisi, na kupeana mikono, na machozi yakitiririka mashavuni mwetu. Na hebu wazia, atakaribia, apanguse machozi yote kutoka machoni mwetu, aseme, “Msilie. Yote yamekwisha sasa. Ingieni katika furaha za Bwana mlizoandaliwa tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu.” Loo, ndugu, hilo litatufanya tupendane zaidi.

⁶⁵ Nafikiri hiyo ndiyo shida ya Kanisa, Bibi-arusi siku hizi, ambaye amefanyizwa kwa makanisa yote yanayomwamini Kristo. Si jengo la kanisa, wala si shirika au dhehebu, bali ni watu mmoja mmoja walio kanisani ambao wanamfanyiza Bibi-arusi.

⁶⁶ Nina rafiki mzuri huko Louisville, Kentucky, Dkt. Wallace Cauble, ambaye alikuwa ni mhudumu wa Kanisa la Kristo, naye alikuja na kumpokea Roho Mtakatifu, naye ni mchungaji wa moja ya makanisa makubwa zaidi, makubwa kabisa katika Louisville, kanisa la Mlango Uliofunguliwa. Amekuwa rafiki yangu wa thamani sana. Na siku chache zilizopita, nilikuwa nimesimama barabarani, nami nikamwona akishuka kuja barabarani. Nami sikuzote nilimpenda, naye alinipenda.

⁶⁷ Lakini siku moja alifanyiwa upasuaji wa mafindofindo, naye alikuwa akitokwa na damu kwa wingi sana. Nao walikuwa wamemweka kule chini kwenye Hospitali ya Mtakatifu Yusufu, nao walisema alikuwa anakufa. Ndipo Bibi McSpadden akanipigia simu, akasema, “Dkt. Wallace Cauble.” Sikumjua bado, bali nilijua kulikuwa na kanisa kubwa la Mlango Uliofunguliwa. Kasema, “Yeye anakufa. Madaktari wamemdunga sindano, kila kitu. Wamemshona. Wakati wote anatokwa na damu, wala hawawezi kuizua hiyo damu. Damu yakote haigandi, na, wajua, kuacha kutoka.” Kisha kasema, “Wana wamishenari mle ndani, nao wanakutaka uje, ukamwombee.”

⁶⁸ Vema, nilikuwa nimesikia juu ya Dkt. Wallace Cauble, na kwa hiyo kwa namna fulani kidogo nilikuwa sipendi, lakini nikaenda kule. Na wakati nilipoangalia kwenye chumba cha hospitali, kulikuwamo na wamishenari na wahudumu mashuhuri, wote mle ndani, wakilia na kuomba. Nami nikawazia, “Loo, jamani! Kakitu kadogo mimi, maskini mtakatifu anayejifingirisha, niingie mle ndani? Afadhali nikae tu hapa nje.” Kwa hiyo nikashuka nikaenda nyuma ya mtambo wa Koka huko nje sebuleni. Nikamwomba Mungu, a—aizue hiyo damu, ya Ndugu Cauble. Nilishuka nikaenda kule chini na kutoka.

⁶⁹ Ndio kwanza nifike nyumbani, yapata dakika kumi na tano, na simu ikalia tena, nao walitaka kujua nimecheleweshwa na kitu gani, kwamba sikuwa nimekwenda huko. Ndipo nikasema, “Ni—nilikuja. Lakini kulikuwako na wengi sana mle ndani. Ni—nilijisikia tu siongozwi kuingia, labda, unaona, wengi sana, wahudumu mashuhuri mle ndani.”

⁷⁰ Ndipo akasema, “Njoo sasa hivi.” Kasema, “Mtu huyu hawezi kuishi ila kwa muda kidogo tu zaidi.”

⁷¹ Kwa hiyo nikarudi kule, tena. Na wakati nilipoingia mle ndani, alikuwa akijaribu kumfanya dada Mkatoliki kumkubali Kristo kama Mwokozi wake; na huku anatokwa na damu, na damu ikitokea kinywani mwake. Nikaingia ndani.

Naye akasema, “Jambo?”

⁷² Nami nikasema, “Jambo?” Alikuwa ameketi kitandani, na akikohoa namna hiyo, na damu ikitoka.

Naye akasema, “Jina lako ni nani?”

Nami nikasema, “Mimi ni Ndugu Branham.”

⁷³ Ndipo akaanza kulia, akanikumbatia kwa mikono yake. Nikapiga magoti pale.

⁷⁴ Sasa, ni Dkt. Wallace Cauble, wa kanisa la Mlango Uliofunguliwa huko Louisville. Mwandikieni barua. “Damu ilikoma sekunde hiyo.” Haijatoka, tangu wakati huo. Unaona? Nasi tumekuwa marafiki wazuri, wazuri sana tangu wakati huo. Na hivi majuzi, nilikutana naye. Naye akasema . . .

⁷⁵ Oswald J. Smith, wengi wenu mnamjua Ndugu Smith. Yeye ni mmishenari mashuhuri, naye huja kwa Ndugu Cauble, kwa sababu anampenda sana. Akasema, “Ndugu Cauble, unajua,” akasema, “Mimi. . .” Jambo fulani kuhusu mke wake. Akasema, “Wakati nilipofunga ndoa kwa mara ya kwanza,” kasema, “nilijisikia kama, vema, kama nikifanya kosa, nitaninii, loo, ninaweza kupata mwingine,” maana alikuwa ni kijana. “Lakini,” kasema, “baada ya watoto kutokea,” kasema, “basi kwa namna fulani ni vigumu kukaa bila huyo mke. Hapo ni unapofikia kwenye umri wa miaka hamsini hivi, kamwe huwezi kuishi bila ya yeye. Na unapokuwa mzee zaidi, mbona, u—unajisikia hivyo.”

Nikasema, “Nadhani hilo karibu ni kweli.” Nilikuwa . . .

⁷⁶ Sababu ya hoja hiyo kutokea, mnajua jinsi akina mama wanavyoweza kununua vitu madukani, na mke wangu alikuwa yumo mle. Naye ni malkia wa hao wote. Anaendelea tu wakati wote. Maskini miguu yangu inauma karibu ya kufa, nikiwa barabarani nikitembea pamoja naye. Naye alikuwa akiniambia, kasema, “Vema, kamwe huwezi kumwacha.” Na hivyo ndivyo tamshi hilo lilivyotokea.

⁷⁷ Nilipoenda nyumbani, nilikuwa nimeketi chumbani, nikiwazia, “Hiyo ni kweli.” Nililitumia hilo kwa kitu kingine.

⁷⁸ Unajua, wakati nilipoongoka kwa mara ya kwanza katika...nilipokuwa mhubiri Mmishenari wa Kibaptisti, niliwazia, “Kama mtu hakuwa Mbaptisti, kamwe hakuwa ameokoka. Hivyo tu basi.” Nami nilibeba Biblia yangu chini ya mkono wangu, nami nilidhani Bwana aliniita kumfanya kila mtu Mbaptisti. “Na kila mtu asiyeamini kama tu Wabaptisti walivyoamini, hawakuwa kwenye picha hata kidogo.”

⁷⁹ Siku ziliposonga mbele, nilidhani kazi yote ilikuwa ni yangu, mimi mwenyewe. Ndipo nikaja kujua, nilimwona ndugu mwingine aliyekuwa na kanisa, mchungaji. Alijitahidi pia, kwa nguvu tu kama nilivyofanya. Hata hivyo, blanketi inatanda kidogo upande wake pia, mwajua.

⁸⁰ Ndipo tunaona, tunahitajiana mmoja kwa mwingine. Na sasa, baada ya sisi kuanza kufikia umbali huu, kwa namna fulani ni vigumu kuishi pasipo mmoja kwa mwingine. Hivyo tu. Inatubidi tu kuwa pamoja, hivyo. Nami ninaamini hilo limo kwenye uamsho huu mkuu wa kipentekoste. Nina furaha kuona viziwi hivyo vya kutojali vikivunjika, Kanisa kuu la Mungu likianza kujiunganisha pamoja katika ushirika. Inamaanisha ya kwamba arusi inakaribia sasa. Na mawe, yakiwa yamekatwa kwa njia ya kipekee, yana nafasi mahali fulani katika jengo hilo, kama ni mawe ya Bwana.

⁸¹ Sasa, ndoa, kwa maana moja, ni mfano. Ndoa ya hapa duniani ni mfano wa ndoa ya mbinguni. Sasa hebu na tulipitie, kwa dakika chache tu, kulisimulia kwa muda mfupi.

⁸² Jambo la kwanza lililopo, inabidi uamuzi ufanywe. Jambo la kwanza, linalotakiwa, katika ndoa ya kawaida, ni kwamba uamuzi hauna budi kufanywa. Msichana huyo hana budi kufanya uamuzi wake, kama anamtaka mvulana huyu; na kijana mwanamume huyo, kama anamtaka msichana huyo. Inabidi uamuzi ufanywe, nawe huna budi kuufanya. Anapaswa awe ndiye mwanamke pekee ulimwenguni unayempenda, naye hana budi kuwa ndiye mwanamume pekee. Kama sivyo, basi ulifanya uamuzi mbaya.

⁸³ Na hivyo ndivyo ilivyo kwa kufanya uamuzi kwa Kristo. Jambo la kwanza unalopaswa kufanya, ni kujiamulia kama utamtumikia Mungu na kumchukua kama Mwokozi wako, ama hutafanya hivyo. Je! utautumikia ulimwengu? Je! utamtumikia Kristo? Inakubidi kuamua. Inabidi uamuzi ufanywe. Unapoamua, kwamba ama utaenda kumtumikia Mungu au mali, ndipo basi unachukua uamuzi wako. Lakini uamuzi hauna budi kufanywa.

⁸⁴ Halafu basi, baada ya uamuzi kufanywa, ya kwamba wewe utamtumikia, ndipo uchumba unafanywa. Hilo, unapata hilo madhabahuni. Inakupasa kufanya uchumba kabla ndoa hii

haijafanyika. Na hivyo ndivyo ilivyo na Kanisa la Kristo. Inabidi iwe ni uchumba na Kristo, a—ahadi, uchumba, uhusiano wa kimapenzi.

⁸⁵ Halafu basi, jambo lingine, ni—ni kufanya ahadi. Inabidi kuahidiana mmoja kwa mwingine, kama vile unavyofanya ahadi. “Mpenzi, kama utafunga ndoa na mimi, ninaahidi ya kwamba nitakuwa mwaminifu na mkweli. Sitamwangalia mwanamke mwingine.” Ama, “Sitamwangalia mwanamume mwingine. Nami nitafanya hayo yote kama wajibu, kama mke. Tukipata watoto, nitafanya yote kama jukumu kama—kama mama. Mimi, nitakuwa mtunzaji nyumba.” Ahadi hizi zote hazina budi kutolewa, ama zinapaswa kutolewa, katika arusi ya kweli.

⁸⁶ Na ni jambo lilo hilo unapomjia Kristo. “Bwana, kama utanipokea katika Ufalme Wako, ninaahidi.” Haya basi. “Nitakupenda. Nitakuwa mwaminifu Kwako. Nitakutumikia, mchana na usiku.” Ni jambo baya sana tunasahau hilo. “Nitakutumikia, mchana na usiku. Nitafunga. Nitaomba. Nitakuwa mwaminifu Kwako. Nitaleta zaka zangu kwenye ghala. Mimi, nita—nitaomba, mara nyingi kwa siku. Nita—nitafanya jambo lolote. Nami nitaahidi upendo wangu wote Kwako.” Hivyo ndivyo unavyopaswa kufanya. Hiyo ni kweli kabisa, ambapo unaahidi jambo hilo, na linapaswa kutoka moyoni mwako.

⁸⁷ Kama ukimwahidi mume wako jambo hilo, wala si kutoka moyoni mwako, unalimaanisha, huishi hata kidogo kwa usahihi naye. Kwa namna fulani ni jambo la uongo.

⁸⁸ Angalia hapa. Kama—kama huna meno, nawe unatumia meno ya bandia, sasa, hilo ni sawa. Unayaweka badala ya meno uliyokuwa nayo wakati mmoja. Ila, kwa kweli, meno hayo hayajaunganishwa nawe. Si sehemu yako. Kama ulikuwa umekatwa m—mkono, na unaweka mkono wa bandia, vema, mkono huo kweli haujaunganishwa nawe. Umebandikwa tu kwako. Unaona? Haujaunganishwa nawe.

⁸⁹ Na wakati tunapomwekea Kristo ahadi zetu, kama hatuwi sehemu Yake, kama vile mwanamke anavyopaswa kuwa sehemu ya mwanamume na mwanamume sehemu ya mwanamke, basi sisi ni Wakristo bandia. Sisi sio Wakristo, kwa kweli. Kweli hujamwoa mwanamke huyo. Huenda ukawa mwaminifu. Kama humpendi mume wako, naye ana umri wa miaka sitini ama sabini, nawe humpendi vizuri kama ulivyompenda hapo mwanzo, basi wewe unawalea tu watoto wake.

⁹⁰ Hivyo ndivyo makanisa yalivyo, mengi mno siku hizi. Tunachukua tu jina la “Kanisa la Kikristo,” tukijifanya kuwa Bibi-arusi. Wakati, ni kibandia. Hatujaunganishwa na Kristo kwa njia yoyote. Sisi ni kama jino la bandia, mkono wa bandia, jicho la bandia. Unaona? Ni kitu ambacho ni cha bandia

kama tunajifanya tu. Vema, huwezi kuiga Ukristo. Unapaswa kuunganishwa nao.

⁹¹ Na halafu kanisa ambalo ni la bandia tu, linaloitwa kanisa la Kristo, vema, hao watoto basi hawamo Mle, waliozaliwa na shirika lilo hilo. Ni ninii tu... Wao si watoto wa Kristo. Ni watoto wa kimadhehebu, wala si watoto wa Kristo.

⁹² Kama mwanamake hajaunganishwa na mwanamume katika uaminifu, basi si mumewe. Ni mwanamume tu ambaye ameweka nadhiri kuishi naye, naye aliweka nadhiri isiyo ya kweli. Aliahidi kumpenda, naye huyo mke alisema alimpenda, wala hakumpenda. Wakati wote, mwanamume huyo amedanganyika.

⁹³ Lakini kuna jambo moja la hakika, enyi marafiki, hatutamdanganya Kristo. Yeye anawajua walio Wake.

⁹⁴ Lakini, unaona, kwanza, maamuzi yanafanywa. Pili, uchumba. Halafu, ahadi.

⁹⁵ Na, halafu, sherehe. Na hapo ndipo bibi-arusi—bibi-arusi anapolichukua jina la bwana arusi. Yeye si wa jina lake mwenyewe tena. Anachukua jina la bwana arusi.

⁹⁶ Ndipo basi wakati Kanisa linapokuwa na sherehe, linapofanya ahadi zao, ndipo linapochukua Jina la Bwana Arusi. Basi si kanisa la ulimwengu tena. Ni Kanisa la Bwana Yesu Kristo. Amina. Si... Simaanishi, hilo, kwa Jina. Ninamaanisha, hilo, kwa Kuzaliwa, kwa maumbile, kwa nguvu za Mungu. Kwa Kweli ya Mungu iliyofunuliwa, moyoni, linakuwa Kanisa la Kikristo, lile Kanisa kuu la Kikristo la kimitume la ulimwenguni kote. Linakuwa sehemu ya Kristo. Linapofanya hivyo, hilo... Kristo anatia ndani Yake Roho Wake mwenyewe, Uzima Wake mwenyewe. Na Biblia ilisema, kwa Adamu na Hawa, pale, "Ninyi si wawili tena, bali ni mmoja." Na wakati mwanamke, Kanisa, linapoolewa na Kristo, wao si wawili tena. Wao ni Mmoja. Kristo ndani yako! Amina. Jambo ndilo hilo. Uzima Wake umetiwa ndani yako, ndipo unakuwa Bibi-arusi.

⁹⁷ Halafu, jambo lingine, baada ya yeye kuweka nadhiri hizi zote, na kadhalika, na sherehe imetamkwa:

⁹⁸ Kama vile, jina la mke wangu lilikuwa ni Broy kabla aolewe. Sasa, yeye si Broy tena. Yeye ni Branham. Sasa, yeye si Broy tena. Yeye ni Branham.

⁹⁹ Na wakati unapoingia katika Kristo, wewe si wa ulimwengu tena. Wewe ni wa Kristo. Unaona? Huyajali tena mambo ya ulimwengu. Yamekufa kwako. "Kwa kuwa yeye aipendaye dunia, au mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yake."

¹⁰⁰ Kwa hiyo, unaona, huwezi kuwa Mkristo bandia. Unaweza kuwa Mkristo bandia, anayekiri.

¹⁰¹ Bali huwezi kuwa Mkristo, kuwa, mpaka Kristo ajiingize Mwenyewe, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, ndani yako. Ndipo

umeunganishwa Naye. Ninyi si wawili tena. Ninyi ni Mmoja. Kristo aliahidi kuwa ndani yetu, kama vile Baba alivyokuwa ndani ya Kristo. “Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Wewe na Mimi ni Mmoja.” Unaona? Kristo ndani yetu! Yote aliyokuwa Mungu, Yeye aliyamimina ndani ya Kristo. Na yote aliyokuwa Kristo, Yeye aliyamimina ndani ya Kanisa, lipate kuendeleza kazi ya Injili.

¹⁰² Ndipo tunakuwa, si kwa jina la bandia, bali kwa uhalisi wa Roho wa Uzima akituunganisha katika Kristo. Ndipo, kupitia nguvu za kufufuka Kwake, tunafufuliwa kutoka katika mambo mafu ya ulimwengu, na kuketi pamoja Naye katika ulimwengu wa Roho. Amina. Ninapenda jambo hilo. Usiku wa leo, tunaketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, unaona, tumefufuka pamoja Naye; tukafa kwa mambo ya ulimwengu, na tukamchukua Kristo. Na tunapomchukua Kristo, basi ulimwengu umekufa, ndipo hatuujali ulimwengu tena. Ulimwengu umekufa kwetu. Nasi tunaninii... Nao umekufa kwetu, nasi tumeufia.

¹⁰³ Wewe ni mtu wa tofauti, utu wa tofauti, kwa sababu wewe ni kiumbe kipya. Kiumbe! Si kiumbe kile kile, kilichopigwa msasa; si m—mtu aliyefungua ukurasa mpya. Bali ni mtu aliyekufa, na amezaliwa tena, na amekuwa kiumbe kipya katika Kristo Yesu, na Roho wa Mungu aliye hai anaishi katika mtu huyo.

¹⁰⁴ Sasa, ni kama tu huyu mwanamke ambaye si Broy tena, yeye ni Branham, naye anajulikana kwa jina hilo.

¹⁰⁵ Nalo Kanisa si la ulimwengu tena, bali liko katika Jina la Kristo, ndivyo lilivyo. Limeunganishwa Naye, kwa Uhai Wake mwenyewe.

¹⁰⁶ Je! ulipata kusoma katika Maandiko, jinsi ambavyo mtu wa kwanza, aliyeumbwa na Mungu, alikuwa mtu mwenye a—asili mbili? Adamu alikuwa Adamu na Hawa pia, tuginena kiroho, lakini wakati Yeye alipomuumba mtu wa kwanza katika sura Yake mwenyewe. “Naye Mungu ni Roho.” Lakini, wakati alipowaweka katika mwili, Yeye aliwatenganisha. Alichukua roho ya kiume, akaiweka ndani ya mwanamume, kisha akachukua roho ya kike na kuiweka ndani ya mwanamke.

¹⁰⁷ Sasa, unapomwona mwanamke akitaka kutenda kama mwanamume, kuna kasoro. Unapomwona mwanamume akitaka kutenda kama mwanamke, kuna kasoro. Kwa hiyo inaonekana kana kwamba ulimwengu umepotoka kabisa, siku hizi. Wanaume wanajaribu kutenda kama wanawake; wanawake kama wanaume. Hiyo ni kweli. Ni kweli.

¹⁰⁸ Sasa angalia. Ni kamilifu kabisa, kwamba wakati Mungu alipomchukua na kumuumba mwanamume, na kuonyesha ya kwamba Yeye hakumtaka atoke kwenye kitu chochote tofauti, mwanamke hakuwa katika ule uumbaji wa asili. Kwa hiyo yeye hayuko kwenye ule uumbaji, bali yeye ni sehemu ya

Adamu. Yeye ni zaotuka. Yeye anaingia ubavuni mwa Adamu, si kuumba kiumbe kingine, bali kuchukua sehemu ya kiumbe na kufanya kiumbe kingine kutoka kwake. Naye alichukua roho ya kiumbe iliyokuwa katika Adamu. . . Na akachukua roho ya kike iliyokuwa katika Adamu, hasa, na kuiweka katika mwanamke. Kwa hiyo, roho pamoja na mwili, vikawa mmoja.

¹⁰⁹ Ilikuwa ni mfano mzuri kwa yale Mungu aliyofanya pale Kalvari. Yeye alimchukua Kristo, kisha akamuunganisha na Kanisa, kupitia kwenye ubavu uliotobolewa, Yeye alileta Damu iliyomsafisha mtu, inayoutakasa mwili wa Kanisa, na kuiweka Roho ya Mungu aliye hai, aliyoitoe pale msalabani, kutoka kwa Kristo, na kuiweka katika mtu binafsi. Ndipo wao ni mmoja. Wanakuwa mmoja. Kristo na wewe ni mmoja.

¹¹⁰ Na wewe na mume wako mnapaswa kuwa mmoja. Kama kuna kitu chochote kinyume, basi ndoa yenu ina kasoro.

¹¹¹ Na kama kuna kitu chochote kinyume nasi, kwa Kristo, hatuamini Neno Lake, tunasema, “Loo, hilo lilikuwa ni kwa ajili ya siku zingine,” muungano wetu Naye una kasoro. Kama ukisema, “Siku za miujiza zimepita; hakuna uponyaji wa Kiungu; hakuna ubatizo Roho Mtakatifu,” unatumia hilo mahali fulani huko nyuma, hilo linaonyesha ya kwamba Roho wa Kristo hayumo ndani yako.

¹¹² Kwa sababu, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili.” Ndipo wakati Neno Lake linapokuwa dhahiri ndani yako, basi, unaona, ni wewe na Kristo ni mmoja basi. “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, mnaweza kuomba mtakalo,” kwa kuwa si ninyi tena. Ni Neno la Mungu, Kristo ndani yenu. Mnakuwa mmoja. Vema.

¹¹³ Halafu, jambo lingine, baada ya yeye kufanya hivyo, baada ya kutimiza nadhiri zake, na kufanya ndoa yake, na kuchukua jina la atakayekuwa mume wake, jina la bwana arusi, ndipo yeye ni mrithi wa kila kitu mume alichochacho. Yeye ni mrithi wa kila kitu. Mke wako ni mrithi wa kila kitu ulicho nacho.

¹¹⁴ Na hilo ndilo jambo Kanisa lililo, kama lingalilijua tu, likiwa ni sehemu Yake pamoja na Roho Wake akiwa ndani yake. Yeye alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Kubwa kuliko hii mtazifanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Basi ni Kristo ndani yenu. Mmeunganishwa pamoja, nanyi ni warithi pamoja Naye.

¹¹⁵ Na kama Yeye angekuwa hapa duniani, angekuwa akifanya nini? Jambo lile lile alilofanya pale, kwa maana ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Angekuwa akijali shughuli za Baba. Angekuwa akiwaponya wagonjwa. Angekuwa akifanya miujiza. Angekuwa akifanya vile vile kabisa alivyofanya alipokuwa hapa

duniani, kwa sababu anadumu yeye yule jana, leo, na hata milele. Ni jambo kamilifu kabisa. Hiyo ndiyo ndoa.

¹¹⁶ Lakini, sasa, vipi kama mwanamke huyu akiolewa, anaweka nadhiri hizi zote na kila kitu, naye anakuwa mume wa mwanamume huyu, naye ni mrithi wa yote mume aliyo nayo, na kadhalika, halafu apotoke? Anaanza kulipuka. Anaondoka, akiwafuata wanaume wengine. Si hilo tu, bali anashiriki mapenzi yake na wengine. Mtu na mkewe, ahadi zote ambazo wamefanya, halafu huyo mke anatoka anaenda na kuanza kushiriki maisha yake na wengine, mapenzi yake na upendo wake na wengine.

¹¹⁷ Hivyo ndivyo watu wengi sana wanaojiita Wakristo wanavyofanya, kushiriki mapenzi yako na ulimwengu: kucheza, kucheza dansi, kucheza kamari, kukaa nyumbani wasihudhurie mikutano ya maombi, wapate kuangalia televisheni, kila namna ya mambo ya ulimwengu ambayo yamechukua mahali pa kumpenda Mungu, katika moyo wa kanisa. Amepotoka ghafla. Ameingia wazimu. Ameenda kuwatafuta wanaume wengine. Anagawa mapenzi yake. Atachukua zaka zake anazopaswa kutoa kanisani; atazitumia katika mambo mengine huko nje ulimwenguni. Ataninii... Badala ya kumpenda Mungu jinsi anavyopaswa kufanya, na kumwishia Mungu, na kupenda kuja kanisani, karibu inakubidi kumshawishi aje.

¹¹⁸ Loo, ninajua, hapa si muda mrefu uliopita, m—mhudumu fulani aliniambia ya kwamba alituma ninii nyingi sana za maombi... kadi nyingi sana, kuwafanya watu watie sahihi, ya kwamba wangeahidi kuja kwenye shule ya Jumapili angalau miezi sita katika kila mwaka.

¹¹⁹ Nami nilikuwa nimemwona maskini msichana mmoja mdogo huko chini ya kilima kule, ambako nilikuwa nikifanya kazi. Naye alitoka akaja kule. Nami nilikuwa nimesimama mlangoni, nikabisha mlango, naye akaja mlangoni. Naye alikuwa baadhi ya hawa wachezaji wenda wazimu hapa, unajua.

¹²⁰ Kama kundi hili walilolazimika kulitia mbaroni hapa chini Phoenix jana usiku, ninaamini lilikuwa ndilo hilo, wakifanya upotovu huu mpya wa—wa roki, ama wanenguaji, chochote kile ulichoitwa, nao iliwalazimu kuwaleta polisi kuwashika. Enyi vijana, hivi hamfahamu ya kwamba hiyo ni roho ya ibilisi? Chini ya ushawishi, mpaka hawakujijua wao ni akina nani, huko nje mitaani, wakifanya maovu.

¹²¹ Kama baadhi ya hawa wacheakeshaji, ama hawa wacheza vinanda vya santuri, na wanamuziki, na kadhalika, wanavyoenda mahali, katika mji niliokuwa. Na wasichana wakitoa nguo zao za ndani na kuzitupa jukwaani, mvulana huyu apate kuzitia sahihi. Hivi hamtambui huyo ni ibilisi? Ni roho wa siku za mwisho. Hakika. Ni aibu sana. Haya basi, wameingia wazimu.

¹²² Msichana huyu, alitoka, akifanya maovu. Hata hakujua nilikuwa... Alisahau nilikuwa nimesimama mlangoni. Naye akasema, "Loo, samahani. Nilisahau jambo la wewe kusimama hapo." Na akamtupia busu jamaa huyo kwenye redio, chochote kile, na kusema, "Nitakutana nawe huko kwenye Green Briar Patch," ama popote pale. Walikuwa wakienda kuwa na namna fulani ya dansi usiku huo.

Basi nikamwambia Dkt. Brown, aliyekuwa rafiki yangu.

¹²³ Akasema, "Kusanyiko lako linaendeleaje huko juu, Billy?"

Nikasema, "Vizuri." Nikasema, "Tunawapa vidonge."

Akasema, "Vidonge vya aina gani?"

¹²⁴ Nikasema, "Injili. Hivyo hakika vinawafanya waendeleo kuja daima." Unaona?

¹²⁵ Naye akaniambia kuhusu jambo hilo, kutia sahihi ahadi hizo. Ndipo nikasema, "Dkt. Brown, unafikiri yule mchezaji mwenda wazimu kwenye ile redio angemfanya yule msichana kutia sahihi ahadi ya kwamba angekuwa kule usiku huo? La hashi. Angeweka rehani nguo alizovaa, apate kufika kule." Kwa nini? Ni kitu fulani ndani yake ambacho kimemuunganisha, roho fulani, kwenye burudani hiyo ya ulimwengu.

¹²⁶ Na mpaka kanisa la Mungu aliye hai, ambalo linaitwa Bibi-arusi wa Kristo, litakapounganishwa na Mungu namna hiyo, lingali litagaagaa ulimwenguni, katika matope ya udongo wa dhambi, mpaka litakapounganishwa na Mungu hivi kwamba, mpaka moyo wake umejazwa sana na utukufu na nguvu za Mungu, mpaka haliwezi kuona kitu kingine ila Kristo. Hiyo ni kweli.

¹²⁷ Hivyo ndivyo itakavyotupasa kufanya. Huo ndio mpango wa pekee, mpango pekee alio nao Mungu, ni kufanya kitu kama hicho. Inakubidi usiingizwe kibandia. Unapaswa kuzaliwa humo, sio kutikiswa uingie humo, ama kuleta barua kanisani. Lakini ni kuzaliwa katika Kanisa la Mungu aliye hai, kwa kuzaliwa upya, kwa nguvu za kufufuka za Yesu Kristo, zinazokufanya kiumbe kipya ndani Yake. Amina. Hilo linalinyosha. Hilo linalinyosha. Hakika. Vema.

¹²⁸ Anaingia wazimu. Anaanza kushiriki mapenzi yake na wengine, mambo ya ulimwengu, burudani za ulimwengu, kwenda mahali pasipompasa kwenda, akisema mambo asiyopaswa kusema.

¹²⁹ Hapa wakati mmoja mimi... Walikuwa na ninii ya akina mama... namna fulani ya karamu ya kanisa orofani. Ilitokea kwamba nilikuwa na jambo fulani la kufanya kwenye orofa ya chini ya nyumba hii. Nami nakwambia, nimesikia mambo mabaya sana nilipokuwa mwenye dhambi, lakini, huo mkutano wa wanawake, sijapata kusikia mizaha mibaya zaidi maishani

mwangu mwote. Ungeweza kuwazia, mtu anayeitwa Mkristo, angeacha uchafu kama huo utiririke toka kwao?

¹³⁰ Huwezi kupata maji matamu na mazuri kutoka kwenye birika lile lile. Unaingiza ndoo kisimani, na inatoka imejaa vifurukuta mikia, tunavyowaita. Ukiingiza ndoo hiyo tena, itatoa kitu kile kile. Birika hilo linahitaji kusafishwa vizuri sana, na kujazwa na maji mazuri.

¹³¹ Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, tukinena kijumla ulimwenguni, kwamba linahitaji kusafishwa kabisa, kujazwa na maji matakatiifu ya Mungu kutoka Mbinguni. Moyo wake umekuwa shimo la maji machafu ya chochote kinachopitia hapo. Lina wapenzi wa kila namna. Biblia ilisema litakuwa nao. “Wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wasiowapenda watu wema.”

¹³² Wakiona mwanamke anayejaribu kuishi vizuri, mwanamume anayejaribu kuishi vizuri, anakuwa “mtakatifu anayejifingirisha,” mama huyo anakuwa “mlokole,” ama kitu fulani cha mtindo wa kale. Ametupiliwa mbali. Anadharauliwa na kukataliwa na watu wa ulimwengu huu. Hiyo ni kweli.

¹³³ Lakini je! ulipata kuona jinsi Kanisa halisi linavyopaswa kufanya? Katika Agano la Kale, walipokuwa na dha—dhabihu, walimchinja ndege mmoja, na kuweka damu ya mmoja juu ya huyo mwingine, mwenziwe aliyekufa; naye akaruka kote duniani, akiinyunyiza damu ya mwenziwe aliyekufa. Wakati Kanisa linapokuwa Bibi-arusi halisi wa Yesu Kristo, litaibeba Damu ya Yesu Kristo, likiinyunyiza ardhini, likisema, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana.” Mazingira yake, yeye kila sehemu yake itakuwa ni ya Mungu. Umbo lake lote litakuwa ni la Mungu. Huwezi kutarajia kitu kingine chochote.

¹³⁴ Hiyo ndiyo sababu watu wanakuja kanisani, pia. Sio kucheza karata na kucheza poka, kucheza densi kwenye orofa ya chini, kunywa supu za jioni na vitu kama hivyo. Hivyo ni vya ulimwengu. Wala hatutaweza kamwe kujilinganisha nao, na tujionee aibu kwa kujaribu kufanya hivyo. Tunapaswa kumhubiri Roho Mtakatifu, katika nguvu, na kufufuka kwa Kristo. Tuna kitu fulani wasicho nacho. Na tukiishi, si kujaribu kuwaiga. Tuishi jinsi tunavyojua ni sawa. Tuishi katika Kristo. Yesu alisema, “Nikiinuliwa juu, nitawavuta watu wote Kwangu. Ninyi ni chumvi ya ulimwengu. Lakini chumvi imepoteza ladha yake, basi haifai kitu bali kutupwa nje na kukanyagwa chini ya miguu ya watu.” Shuhuda zetu!

¹³⁵ Si ajabu, hata makundi yetu ya Kipentekoste, ingawa ninachukia kusema jambo hilo, makundi yetu ya Kipentekoste yanaanguka moja kwa moja kwenye kitu kile kile, moja kwa moja kwenye mtindo ule ule. Na si ajabu watu wanasema hawana kile wanachosema wanacho. Kanisa hili la uamsho wa kipentekoste linapaswa kufungwa pamoja kwa nguvu za

Mwenyezi Mungu, mpaka Uzima ule ule wa Yesu Kristo ungeakisiwa ndani Yake.

¹³⁶ Bali tunataka kujilinganisha na ulimwengu. “Tutafanya hivyo, hata hivyo.” Unaona? “Tunataka kufanya tupendavyo kulihusu.” Lakini haitupasi kufanya hivyo. Ni makosa kufanya hivyo. Makanisa ni kama tu mwanamke, yaliingia wazimu.

¹³⁷ Jambo la kwanza unajua, linakuwa sawa, hapo mwanzo wakati Mungu alipolizaa Kanisa hili la kipentekoste, yapata miaka arobaini ama hamsini iliyopita. Liliishi maisha matakatifu. Lilikuwa takatifu. Nguvu za Mungu zilikuwa pamoja nalo. Lakini tunaposonga mbele, tunaanza kupatana na ulimwengu.

¹³⁸ Muda si muda unajua, lazima tuwe na jengo ambalo ni kubwa sana halina budi kulishinda la Wamethodisti kule pembeni. Hatuna budi kuwa na kitu fulani kikubwa sana, kitu kikubwa kuliko vingine, na kitu kilicho kikubwa kuzidi vyote, na kitu kilicho kikubwa kuzidi vyote. Ni aibu. Wengi wetu tunajigamba tunapofikia...Ndugu Mpentekoste anamwona mtu fulani kule chini, ile misheni ndogo, ama kanisa dogo sana, nao wanahudhuria kanisa kubwa. “Sisi ni wafuasi wa kanisa la kwanza, ama kanisa lile kubwa,” ama kitu kama hicho; anawadharau.

¹³⁹ Unachohitaji ni Roho Mtakatifu, kukutoa majivuno kidogo, hiyo ni kweli, kukujulisha ya kwamba ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu utamfanya mwenye suti nzuri amkumbatie aliyevaa ovaroli na kusema, “ndugu.” Kweli. Wakovu halisi wa mtindo wa kale, nguvu za Mwenyezi Mungu, naam, bwana, zitaifanya maskini nguo ya hariri kuikumbatia kaliko, na kusema, “Dada, ninakupenda.” Hakika itafanya hivyo.

¹⁴⁰ Lakini tunaanza kutoka nje na kwenda kutembea na ulimwengu, tunachukuliwa na mkondo wa maji. Kanisa letu limepeperushwa. Haitulazimu kuzungumza juu ya Wamethodisti na Wabaptisti tena. Ni sisi wenyewe. Liko kwenye tabaka letu wenyewe. Hiyo ndiyo sababu Roho Mtakatifu hawezi kufanya kazi. Hiyo ndiyo sababu ninasema ya kwamba Mungu hawezi kuweka idhini Yake juu ya shirika lolote usiku wa leo. Kwa sababu, Mataifa hawakutolewa kama taifa. Walikuwa ni watu kutoka katika Mataifa, kwa ajili ya Jina Lake. Mungu atawachukua watu binafsi.

¹⁴¹ Sasa, nafikiri mashirika yetu yanafanya kazi nzuri. Hilo ni sawa. Bali huwezi kutegemea jambo hilo, kusema, “Mimi ni mpentekoste, maana mimi ni mfuasi wa dhehebu la Kipentekoste.” Wewe ni Mpentekoste wakati unapopata tukio la kipentekoste. Sijali kama wewe ni mfuasi wa kanisa Katoliki, wewe ni mpentekoste. Huwezi kuiundia pentekoste dhehebu. Pentekoste ni tukio, si dhehebu. Na hiyo ni kweli.

¹⁴² Lakini sisi Wapentekoste tumeanza kufikiria, kwa kuwa tuna jina la Pentekoste, tunaweza kuendelea na kuishi ulimwenguni, kufanya lolote tunalotaka. Ni kana kwamba tunapanda mnara wa Nimrodi; utageuka majivu. Kama vile aproni ya Adamu ya tawi la mtini; litarudi huko. Kama vile ngome ya Siegfried huko Ufaransa, ngome ya Maginot huko Ujerumani; iliporomoka.

¹⁴³ Maana, hakuna mnara mwingine, hakuna msimamo mwingine. “Isipokuwa Jina la Bwana ni ngome yenye nguvu ambayo wenye haki wanaikimbilia na wanakuwa salama.” Unapoikimbilia, unalichukua hilo Jina, hilo Jina; sio tu kuita Jina fulani, bali Jina na jinsi ulivyo wewe, unafanana na Kristo katika maisha. Amina. Yeye ni wa ajabu. Naam.

¹⁴⁴ Kanisa limefanya jambo lile lile, limefanya uasherati wa kiroho, kama mwanamke ambaye angegawa mapenzi yake kutoka kwa mumewe kwenda kwa mwanamume mwingine. Huyu mwanamke hafai kuishi naye. Mnajua hivyo. Na wakati kanisa linapoanza kushiriki ushirika wake na ulimwengu, Mungu ni Mungu mwenye wivu. Aliwaacha Israeli kwa sababu ya jambo hilo, na Mwanawe atakiacha kitu hicho hicho.

¹⁴⁵ Yeye atakuwa na Bibi-arusi asiye na kunyanzi ndani Yake. Amina. Ameoshwa kabisa kwa Damu Yake mwenyewe. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo tunaona mahali tunaposimama, ile arusi ikijiandaa kuja.

¹⁴⁶ Sasa, tunaona ya kwamba yeye anafanya uasherati wa kiroho, kutembea na ulimwengu, anakiri kitu fulani, akiishi kitu kingine tofauti. Hilo kamwe halitafaa kitu. Kile kanisa linachopaswa kufanya, ni kufanya kama Esta alivyofanya. Esta alikataa kujipamba kwa ulimwengu.

¹⁴⁷ Tunakijua kitabu hicho kidogo cha Esta, jinsi ambavyo Mordekai... Mjomba wake alikuwa na binti. Naye alikuwa huko katika wakati wa utawala wa Wamedi na Waajemi. Ni mfano mzuri sana pale. Yule mfalme, mmoja wa wafalme waliokuwa wakuu sana ulimwenguni siku hiyo, alikuwa na karamu kubwa. Naye akamwita malkia aje aketi karibu naye, bali asingefanya hivyo. Alikataa kufanya hivyo. Kwa hiyo alifanya nini? Aliaibishwa sana, hakujua la kufanya, kwamba mke wake mwenyewe asingekuja.

¹⁴⁸ Nafikiri hilo kabisa ni kama Kristo siku hizi. Kristo ametualika kuketi katika ulimwengu wa Roho pamoja Naye, nasi tunauonea aibu. Watu wengi wanaona aibu kusema ya kwamba wana ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wapentekoste, hiyo ni kweli, wanaona aibu kusema hilo. Tunamwonea aibu.

¹⁴⁹ Na kwa hiyo huyo malkia asingekuja. Alikataa kuja. Ilimwaibisha. Uso wake uligeuka ukawa mwekundu. Kila mtu aliona.

¹⁵⁰ Sijui kama uso wa Yesu haugeuki kuwa mwekundu kidogo, pia, wakati anapotuitia kazi, anauitia uamsho wa Kipentekoste ushirika na udugu, nasi tumejiundia madhehebu sana katika makundi madogo madogo hata hatutamwinamia mwingine. Tunaninii sana, tunakuwa wa kilimwengu sana na vitu kama hivyo, tunalionea aibu jina la pentekoste. Watu wengine wanaogopa kusema. Kusema, “Vema, mimi—mimi ni mfuasi wa . . . Mimi ni Mkristo, lakini. . .” Nina furaha nilipata tukio la kipentekoste. Amina. Nina furaha kulichukua Jina la Yesu Kristo. Ndiyo majaliwa makubwa sana niliyopata kuwa nayo, kusema mimi ni sehemu Yake.

¹⁵¹ Sasa tunaona ya kwamba, basi, alipata washauri fulani, kuwauliza anapaswa kufanya nini. Nao wakasema, “Kama jambo hili likiendelea namna hii, wanawake wengine wote kote nchini watachukua mfano wa mama taifa.”

¹⁵² Bila shaka, hivyo ndivyo inavyotendeka usiku wa leo. Ninawaangalia baadhi ya wanawake hawa. Natumaini siziudhi hisia zenu, na hata hivyo ninawaudhi, natumaini ninawaudhi. A-ha. Naam. Wakijaribu kuwa kama upuuzi huu hapa wa mama taifa, wakiwa na huku kukata nywele kichwamaji. Sijapata kuona kitu kama hicho maishani mwangu mwote.

¹⁵³ Hivi majuzi kulikuwa na mwanamke aliyekuja kwenye duka nilipokuwa nikimngojea mke wangu, na kichwa cha mwanamke huyo kilikuwa kikubwa *hivi*, naye alikuwa na rangi ya kijanikibichi chini ya macho yake. Nikasema, “Rudi nyuma, ewe bugi. Nitakuwa mzuri.” Kilikuwa ni kituko cha ajabu. Kingekushtusha sana. Ni kitu gani? Mama wa taifa. Ni mama wa taifa. Mambo ndiyo hayo. Nao wanachukua mfano kutokana na hilo.

¹⁵⁴ Na hebu niseme jambo hili sasa. Sikulisema kimzaha, bali katika mfano, mpate kuona. Hivyo ndivyo hasa ambavyo ninyi Wakristo wa siku nyingi mnavyofanya kwa hawa wachanga. Kweli kabisa. Mnapaswa kuwa mifano. Ninyi Wapentekoste mnaokiri kuwa na Roho Mtakatifu, mnapaswa kuwa mfano kwa Wamethodisti, na Wabaptisti, Wapresbiteri. Sio kama mama wa taifa, bali mnapaswa kuwa kama Yesu. Yeye anawaambia la kufanya *Humu* ndani, jinsi ya kulifanya. Inatupasa kufuata sheria na mifano Yake. Bali hivyo ndivyo tunavyolikuta. Esta . . .

¹⁵⁵ Malkia huyu, asingesikiliza jambo hilo. Asingekuja; alimwaibisha. Kasema, “Kama—kama huyu mama wa taifa wa nchi akiweka mfano wa namna hiyo, wanawake wengine wote watafanya hivyo. Kwa hiyo basi wakati mwanamume anapomwita mkewe, yeye atasema, ‘Nenda kajirushe mtoni.’” Unaona? Jamani, yeye kweli aliitabiria Marekani, sivyo? Sasa, tunaona ya kwamba, katika kufanya jambo hilo, ndipo kulikuwa na mtu aliyekuwa na hekima kidogo, akaja na kushauriana na mfalme. Akasema, “Jambo la kufanya ni kumwondosha. Kisha

upige mbiu kote nchini, na kuwaita mabikira wote walioko, mabikira vijana, na hapo ukajichagulia mke.”

¹⁵⁶ Lilimpendeza mfalme. Kwa hiyo akawatuma, naye akawatuma wahudumu wa kike, na kadhalika, ambao walitoka wakaenda ku—kuwachukua mabikira wote wadogo walioweza, wanawake warembo kote katika falme zote na majimbo aliyoyatawala, ambao ulikuwa ndio mkubwa sana ulimwenguni.

¹⁵⁷ Na wakati alipofanya hivyo, lilimpata huyu msichana mdogo wa Kiyahudi. Alikuwa kwa namna fulani aliyetelekezwa, kwa sababu, kama vile Mataifa, unaona, alitelekezwa kwa upande mmoja. Naye hakuwa na baba wala mama. Na Mordekai, mjomba wake alikuwa akimlea. Naye ilimbidi kwenda, kustahimili.

¹⁵⁸ Na kwa hiyo kile walichofanya, ilibidi wawachukue wasichana hawa kwa ajili ya utakaso kwa miezi kadhaa. Iliwabidi kuwatia marashi na kufanya kila namna ya kuwarembesha, na kuwatengeneza sawasawa, wapate kwenda mbele ya mfalme.

¹⁵⁹ Sasa, hivyo ndivyo kama vile ulimwengu unavyotaka kulirembesha kanisa siku hizi. Kulirembesha na mambo ya ulimwengu; kulilinganisha na mambo ya ulimwengu; kujaribu kupata wafuasi zaidi, wakiingiza chochote kile katika ushirika wao. Jamani! Ni jambo la kuhuzunisha. Dhehebu moja linajaribu kushinda lingine, kuingiza kitu chochote kuwa mfuasi wake. Unaweza kuwaingiza katika dhehebu hili, bali kamwe hawataingia katika ushirika wa Kristo mpaka watakaposafishwa na kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Hiyo ni kweli. Huenda wakaandika jina lao katika kitabu hapa, bali si huko Juu, kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, mpaka litakapoandikwa kwa Damu ya Bwana Yesu.

¹⁶⁰ Wanawake wote, walijipamba vizuri, wapate kuonekana warembo. Na, loo, ninawazia walijirembesha kwelikweli, labda kujifananisha na mama wa taifa na kadhalika. Walijiandaa vyema kabisa kwa sababu walikuwa waende kuonekana mbele ya mfalme.

¹⁶¹ Nafikiri hivyo ndivyo karibu inavyokuwa kwa makanisa yetu ya siku hizi. Yanajaribu kujirembesha vizuri sana, kilimwengu, yakiwa na burudani za kilimwengu, mambo ya ulimwengu ndani yake, yakifanya mambo ambayo ni ya ulimwengu, kujihusisha na ulimwengu, yakidhani yanaweza kukutana na Mfalme. Mungu hajali kuhusu mambo hayo. Anayachukia hayo. Lakini tunataka kutenda kama ulimwengu.

¹⁶² Baadhi ya makanisa yetu, nimesema, yanalegeza mambo, yakiwachukua mashemasi, na kadhalika, katika kanisa, na wakati mwingine wachungaji, ambao wameoa mara nne ama tano, na—na baadhi yao ambao wanavuta sigara. Wanasema,

“Wata—wataondokana na jambo hilo. Watakuwa sawa.” Wanamtoa mtu kutoka kwenye kilabu cha pombe usiku mmoja, na kumweka mimbarani kesho yake usiku. Siamini katika upuuzi kama huo. Ninaamini mtu anapaswa kuthibitishwa, hiyo ni kweli, kuthibitishwa. Nawaambia, mara nyingi tunaita . . .

¹⁶³ Ninaamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ninaamini katika kunena kwa lugha, lakini nafikiri tunatilia mkazo sana jambo hilo. Mtu anaweza kunena kwa lugha, na mwanamke anene kwa lugha, na kama maisha ya mwanamke huyo na mwanamume huyo hayalingani na lugha unazonena, basi ni lugha za uongo, maana Roho Mtakatifu atakufanya utende kama Biblia. Atakuleta kwenye utimilifu wa kimo cha Kristo.

¹⁶⁴ Hebu chukua mtu anayenena kwa lugha, hasira za kutosha kupigana na msumeni uvumao, na kuwanenanena majirani, na kila kitu namna hiyo. Loo, ati unamwita huyo Roho Mtakatifu? Hawezi kuwa. La, bwana.

¹⁶⁵ Roho Mtakatifu ni upole, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, utu wema, subira, uaminifu. Roho Mtakatifu, hilo ndilo tunda la Roho, ambalo Roho Mtakatifu huzaa katika Kanisa la Mungu aliye hai, uungwana, na unyenyekevu, upole, kupendana mmoja kwa mwingine, uvumilivu.

¹⁶⁶ Kama ndugu amekosea, usimpige papo hapo ama kitu kama hicho. Mwendee uone kama unaweza kumrudisha. Usingojee mhubiri afanye hivyo. Wewe lifanye, mtu mwingine. Mhubiri hawezi kufanya hayo yote, wala mashemasi. Kila mtu, aliye mshiriki wa Mwili huu wa Kristo, wanapaswa kuendeana mmoja kwa mwingine. Tunaninii . . . Na kama tuna Roho wa Kristo ndani yetu . . . Yeye alifundisha ule mfano mkuu. Waliwaacha tisini na tisa, wakamwendea huyo mmoja. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Lakini tunasema, “Loo, achana nao.” Haitupasi kufanya hivyo kamwe. Tunapaswa kuwa na utu wema, wenye kusamehe, wavumilivu. Hilo ndilo tunda la Roho.

¹⁶⁷ Sasa, tunajikuta wenyewe basi, ya kwamba Esta, baada ya yeye . . . Walimweka katika moja ya mahali hapa, apate kurembeshwa kabisa, kumfanya akajionyeshe mbele ya mfalme. Jamani! Alikataa jambo hilo. Hakulitaka. Alitaka kutoka aende kama tu alivyokuwa. Amina.

¹⁶⁸ Tuna makanisa siku hizi ambayo yanataka kutenda kama ulimwengu, ama kwa kuwa tunakuwa wakubwa. Mungu alisema, “Wakati mmoja alikuwa mdogo, walimtumikia. Bali alipokuwa mtu mzima, basi walimsahau.” Hiyo ni kweli.

¹⁶⁹ Tulipokuwa na sufuria ya bati hapa chini kwenye vichorochoro mahali fulani, tukiwa na tari, tukilipiga kwa upande wa nyuma wa mikono yetu; na gita kuukuu, tukalipiga; na tukifanya mkutano wa mtaani, mlikuwa wanyenyekevu. Lakini tunapofikia kuwa na majengo ya dola milioni tatu au nne, na mambo makubwa mno namna hiyo, basi tunakuwa na

majivuno sana hata tunasahau hilo, hiyo ni kweli, tunang'ara tukifanana na ulimwengu.

¹⁷⁰ Nilikuwa mahali fulani hivi majuzi ambapo, ndugu mmoja wa utakatifu, kulikuwa na kundi la watu wakimfanyia kazi. Na kama kila mwanamke alipotoka pale wakati wa kahawa, kupumzika wakati wa kahawa, kila mwanamke pale ndani alikuwa na nywele fupi na amepaka rangi mdomoni. Sasa, unasema, "Ndugu Branham, si kazi yako kusema jambo hilo." Ni kazi yangu. Biblia inasema hivyo. Hiyo ni kweli.

¹⁷¹ Wanawake wengi wa Kipentekoste wanavaa nguo zinazompasa mwanamume, na Mungu alisema ni chukizo machoni Pake. Hiyo ni kweli. Unatarajiaje kwenda Mbinguni namna hiyo? Inaonyesha ya kwamba Roho Mtakatifu hayumo humo. Kama Roho Mtakatifu angelikuwa humo ndani, Yeye angekuhukumu. Kweli. Loo, huenda ukapaza sauti, ukanena kwa lugha, ukakimbia huku na huko, ukacheza katika roho. Nimewaona Wahindu wakifanya hivyo, na Wahindi, na chochote kile. Hilo halimaanishi kitu, isipokuwa pawe na maisha ya kuunga mkono kile unachozungumzia, nguvu za Roho Mtakatifu, kuwafanya watu wanaoishi kitauwa. Huyu ndiye Bibi-arusi wa Kristo.

¹⁷² Esta alikuwa awe bibi-arusi, kwa hiyo hakutaka mapambo yoyote ya ulimwengu. Alitaka kuingia, kupitia kwa mfalme, jinsi tu alivyokuwa. Alijipamba jinsi wanawake wa kipentekoste wanavyopaswa kujipamba, kwa roho nyenyekevu ya upole. Na wakati mama wa taifa hawa wote warembo, walipopitia pale, wakiwa na dansi lao la kisasa na mambo kadhaa, mfalme aliwaangalia, na kuwaweka chumbani pamoja na masuria. Lakini wakati huyu Esta alipokuja mbele zake, naye akapata kutazama kidogo hiyo roho nzuri, nyenyekevu, pole, alisema, "Huyo ndiye. Nenda kalete taji ukaiweke juu ya kichwa chake." Jambo ndilo hilo.

¹⁷³ Hebu wajipambe kwa roho wa aina hiyo, si wanawake tu, bali wanaume pia, wajipambe kwa roho wa aina hiyo. Ndipo unajiweka tayari kwa ajili ya Bi—Bibi-arusi, mpole, mwenye kicho. Esta aliusafisha moyo wake.

¹⁷⁴ Kuna mambo mengi tunayoshughulikia, huu wa nje, loo, unapaswa kuwa na viondoa makunyazi kadhaa, na kiasi fulani cha *hiki*, ku—kuushughulikia.

¹⁷⁵ Hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa nimesimama kwenye jumba la ma—makumbusho huko Tennessee. Nilipita mahali padogo, napo palionyesha uchanganuzi wa mwili wa mwanadamu. Ulisema mtu aliye na uzito wa ratili mia moja na hamsini, katika kemikali alikuwa na thamani ya senti themanini na nne. Sasa, ati wewe ni mtu fulani, sivyo, senti themanini na nne? Na baadhi ya wanawake wataninii, wanawake wa Kipentekoste, watavaa koti la dola mia tano la sufu ya minki

na kuinua kichwa chao, kama ilinyesha, wangekufa maji, na hata hawana thamani ya senti themanini na nne, hiyo ni kweli, katika kemikali. Hiyo ni kweli, si mzaha. Hiyo ni kweli. Senti themanini na nne, karibu rangi ya kutosha kupaka kiota cha kuku, na kalisi kidogo na kadhalika. Senti themanini na nne, angalia jambo hilo kwa makini sana.

¹⁷⁶ Unaenda kwenye mkahawa na kukuta... unapata bakuli la supu na kungekuwa na buibui ndani yake, ungeushitaki mkahawa huo.

¹⁷⁷ Lakini utamruhusu ibilisi akuingizie maskini televisheni chafu na vitu vya karata ndani ya shingo yako, na unayameza; anakufanya kuvaa maskini nguo chafu, hawa wanawake, maskini nguo hizi ndogo zinazobana kama mnyama aliyechunwa ngozi, na kutembea hapa nje mtaani namna hiyo. Na je! wajua, dada yangu, sisemi jambo hilo kwa mzaha. Unanielewa vibaya.

¹⁷⁸ Sikiliza. Ninasema jambo hili. Unafanya hivyo, na kwenye Siku ya Hukumu utahesabiwa kama mzinzi. Kweli. Yesu alisema, "Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake." Na wakati mwenye dhambi huyo atakapopaswa kujibu kwa ajili ya kuzini, ni nani? Wewe. Ni nani aliyesababisha jambo hilo? Wewe. Hiyo ni kweli. Kama ukijianika huko nje, kuonekana mbele ya wanaume, kuwa kama mlimwengu na kuvaa kama walimwengu.

¹⁷⁹ Nilisema hilo wakati mmoja, basi mwanamke mmoja, Louisville, Kentucky, akasema, "Vema, sikiliza hapa, Bw. Branham. Nitakufahamisha sasa hivi!"

Nikasema, "Naam, mama?"

Akasema, "Hizo ndizo aina za nguo tu wanazoshona."

Nikasema, "Wanatengeneza charahani na kuuza vitambaa."

¹⁸⁰ Ni kwa sababu unataka kufanya hivyo. Kuna kasoro fulani ndani yako. Hiyo ni kweli kabisa. Unafanya hivyo siyo kwa sababu ni mtindo. Unafanya hivyo si kwa sababu inakubidi kufanya hivyo. Unafanya hivyo kwa sababu unataka kufanya hivyo.

¹⁸¹ Unavuta sigara kwa sababu unataka kuvuta. Si lazima uvute. Nafikiri jambo la kipumbavu kabisa nililopata kuona ni mwanamke akienda barabarani, kama unavyomwona kila mtu, gari, wakiwa na hizo sigara katikati ya vidole vyao. Mbona, ni fedheha. Huo ndio mwenendo mkubwa mchafu kabisa wa vibaraka wasaliti tulio nao nchini, wakati madaktari na sayansi ya matibabu inasema zimejaa kansa na kila takataka. Nao wanazinyonya moja kwa moja, wakati wote.

¹⁸² Unamwona mwanamke, anayeaminiwa kwamba ni Mkristo, amejilaza pale ufukoni, wanakoogelea watu mchanganyiko, amevaa suti ya kuogelea, amejilaza hapo. Nina wasichana wawili. Sisemi hawatafanya hivyo. Wanasema wanajibadilisha

rangi kwa kuota jua. Watapata badiliko la mwana kama nitakuwa hai. Itakuwa ni mwana wa *hii*. Unaona? Itakuwa ni mwana wa Bw. Branham, akiwa na ubao mrefu *hivi*. Ninaamini ni makosa.

¹⁸³ Halafu tunajiita wenyewe, “Loo, sisi ni wafuasi wa kanisa la Kipentekoste.” Loo, mnatia aibu! Kweli. Kanisa la Kipentekoste linahitaji kusafishwa, kote kutoka mbele mpaka nyuma, na kupitia kwenye ghala iliyo chini ya ardhi na chumba cha chini ya ardhi, na ghorofani. Hiyo ni kweli. Na hata hivyo, katika yote hayo, ndilo zuri zaidi tulilo nalo. Lakini linaweza. . .

¹⁸⁴ Ni kama tu katika yale mapinduzi na katika wakati wa Joan wa Arc, Ufaransa ilihitaji mapinduzi, basi wanahitaji mapinduzi ya pili kuyapindua hayo mapinduzi wapate kunyosha baadhi ya mambo waliyokuwa wakiasi.

¹⁸⁵ Nalo kanisa la Kipentekoste linahitaji mapinduzi. Kweli. Hakika linahitaji. Kuasi mambo ambayo ni mabaya, na kukubali mazuri, amina, ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu: “Kanisa kujifanya tayari Lenyewe!”

¹⁸⁶ Kumbukeni, kamwe haitakuwa. . . Huwezi kusema, “Vema, sasa, mimi ni mfuasi wa *hili*, Assemblies. Mimi ni mfuasi wa Foursquare, ama Kanisa la Mungu, ama Jina la Yesu,” ama—ama lolote la hayo mengine. La! Huwezi kuingia kwenye lolote la hayo.

¹⁸⁷ Mungu hukuita wewe kama mtu binafsi. Na ni wewe ndiwe unayepaswa kujitakasa, kwa sababu, “Yeye anawachukua watu kutoka kwa Mataifa, kwa ajili ya Jina Lake, Bibi-arusi Wake, Mmataifa.”

¹⁸⁸ Esta alijitakasa. Aliutakasa moyo wake. Huo ndio aliosafisha. Hicho ndicho kanisa linachohitaji: kusafishwa kwa moyo.

“Unautakasaje moyo wako, Ndugu Branham?”

¹⁸⁹ “‘Kuoshwa kwa maji ya Neno,’ kwa Damu ya Yesu Kristo.”

¹⁹⁰ Biblia ilisema ni makosa kwa mwanamke kufanya hivyo, na kwa wanaume kuwaacha wafanye hivyo. Hilo ni nyote wawili. Mwanamume atakayemwacha mke wake atoke aende barabarani akiwa na ninii uchi, akiwa na nguo za aina hiyo, nina heshima haba kwake hata kuwa mwanamume. Yeye ni kibaraka. Hiyo ni kweli. Mkewe anamtumia kama kitambaa cha kupangusia vyombo. Mnatia aibu. Mnapaswa kuwa wanaume.

¹⁹¹ Na mchungaji ataliachilia kanisa lake lifanye mambo kama hayo, bila ya kulikemea vikali sana kutoa lami hiyo kutoka mimbarani. Yeye ni dondoadume. Tunachohitaji ni wanaume, Injili, si kwa glavu za mpira, bali kwa nguvu na dhihirisho la Roho Mtakatifu, pamoja na Neno. Biblia inasema mambo haya ni makosa. Ni vibaya kwa watu kufanya hivyo, kutenda

hivyo. Linapaswa kuhubiriwa, na kuishiwa, na kila mahali. Vinginevyo, kanisa linahitaji kutakaswa, kusafishwa kabisa.

¹⁹² Esta aliutakasa moyo wake mbele za Mungu, alienda kule kwa moyo wa upole na roho mnyenyekevu; Kanisa ambalo litakuwa Bibi-arusi wa Kristo. Sasa, kumbukeni, Esta alikataa mapambo ya ulimwengu. Alimchukua Roho moyoni mwake, kwenda mbele ya mfalme.

¹⁹³ Na mwanamke siku hizi, kanisa linalodhania litaenda kuingia kwa sababu lina wafuasi wengi zaidi, ndilo lenye umati uliovalia vizuri kuliko yote, lina dhehebu lililo kubwa zaidi, kanisa lililo kubwa kabisa jijini, na mambo kama hayo, utakosa hilo maili milioni moja kama unategemea hilo.

¹⁹⁴ Ni roho mtamu, mwema, mwenye kicho kwa Neno la Mungu, “aliyeoshwa kwa maji ya Neno,” na Neno limo ndani yako. Ni kuoshwa. Amina. Kanisa linahitaji kuoshwa, kuoshwa na Injili yote. Hiyo ni kweli. Sio kuoshwa kwa sehemu tu, bali kuoshwa kwa Injili yote, limeoshwa kinaganaga, “kufanywa viumbe vipya katika Kristo Yesu.”

¹⁹⁵ Bibi-arusi wa Kristo si bibi-arusi mchafu. Yeye hatakuwa na Bibi-arusi Wake, mchafu.

¹⁹⁶ Kama mwanamke akija kuolewa, naye alionekana kana kwamba ametoka kwenye zizi la nguruwe huko nje; mwanamume aliye mwenye heshima yoyote, asingemwoa. Angemfanya aoge vizuri.

¹⁹⁷ Na wakati kanisa la Kristo linapokuja kuolewa, linafikiri litaingia katika Bibi-arusi, likiwa na sifa zote za ulimwengu juu yake, Bibi-arusi wa Kristo hatakuwa hivyo. La, bwana.

Inanibidi kuharakisha.

¹⁹⁸ Wala Kanisa la Kristo, la Bwana Yesu Kristo, wala Kanisa hilo si kanisa lililovaa marapurapu, wala, lililo na matambaa yaliyochakaa ya madhehebu. Si lazima liwe mwanachama wa dhehebu fulani kubwa. Linapaswa kuwa limeoshwa kwa Damu, kununuliwa kwa Damu. Sio kusema sisi ni wafuasi wa kanisa lililo kubwa kuliko yote, dhehebu lililo kubwa kuliko yote, ama *hili*, *lile*, ama *linginelo*. Linapaswa kuwa safi, lililotakaswa, takatifu, bila waa wala kunyanzi, kwa damu ya Mwokozi wa—wake, Yesu Kristo.

¹⁹⁹ Kama vile Esta, yule Mtu aliyefichwa moyoni, yule Mtu aliyefichwa, upole na unyenyekevu wa Roho wa Mungu, katika moyo wa mwanadamu; sio utukufu na tabaka la ulimwengu.

²⁰⁰ Daima nimesema ulimwengu hung’aa; bali Injili humeka. Loo, zimeachana kwa maili milioni moja. Hollywood hung’aa; Kanisa la Kristo humeka kwa uzuri, na ni jororo, na tamu, jema. Hiyo ni kweli.

²⁰¹ Esta hakutaka kujipamba kwa mapambo yote ya kisasa ya ulimwengu. Huyu asingonekana kama mke wa mfalme.

²⁰² Nasi, kutaka kuwa kama ulimwengu, na je! huyo angeonekana kama Mke wa Mtu Mtakatifu? Ati sisi, kama Kanisa la Mungu aliye hai, kujipamba kwa vitu vya ulimwengu, na halafu tuonekane kama Mke wa Mtu Mtakatifu? Je! huyo angeonekana wa maumbile ya kiasili?

²⁰³ Kama ungemwona mtu siku hizi, ambaye anadhaniwa kuwa ni mtu mtakatifu; huyu hapa mke wake anakuja, kama mama wa taifa, akiwa na moja ya hiyo mitindo iliyotukuka ya nywele namna *hii*; na kitu chekundu upande mmoja, na cha kijani kibichi upande huo mwingine, na—na anaonekana kana kwamba ameguswa mdomoni kwa brashi ya kupaka rangi; na mambo kama haya yote ya namna hiyo, akitembea barabarani, amevaa nguo fupi zinazombana kama mnyama namna hiyo; na visigino virefu *hivi*, akienda kwa kukatikakatika, akitembea kwa hatua za madaha barabarani; na ati useme, “Huyo ni mke wa mtu mtakatifu”? Sifanyi mizaha. Ninatoa tu matamshi.

²⁰⁴ Nilikuja kwenye mmoja wa miamsho yetu mikuu ya Kipentekoste, hapa si muda mrefu uliopita. Nilikuwa nimepiga hema. Na huyo mchungaji akaniambia, kasema, “Mke wangu ndiye mpiga kinanda.”

Nikasema, “Hilo ni jambo zuri, ndugu.”

“Utajali yeye akikipiga?”

Nikasema, “La. La, bwana. Hakika sijali.”

²⁰⁵ Basi akamwendea meneja. Meneja akasema, Ndugu Baxter, akasema, “Hilo ni sawa.”

²⁰⁶ Akasema, “Ndugu Branham, njoo hapa. Ninataka ukutane na mke wangu.” Nami nikaenda pale.

²⁰⁷ Naomba mnisamehe. Mnaona? Sijaribu, kutoa ta—tamshi kwa ajili yetu sisi. Ninajaribu kusema jambo fulani. Mnaona?

²⁰⁸ Na mwanamke huyo alikuwa na moja ya hizi rangi za makucha. Sijui. Takataka hizo, mwajua, amejipamba kwelikweli, nami sijapata kuona kitu kama hicho maishani mwangu; na nguo iliyokuwa chini sana *hapa* ndani, haina upande wa nyuma, na karibu haina sehemu ya chini. Nami si—sijapata kuona tamasha kama hilo maishani mwangu. Naye alikuwa na vipuli vikubwa sana vikining’inia chini namna *hii*, na amevaa vitu vingi sana.

²⁰⁹ Nami nikaangalia kote. Nikawazia, “Loo, jamani mimi!” Mimi ni Mbaptisti, nami ninajua vizuri zaidi ya hivyo. Nikaangalia tena. Nikasema . . .

²¹⁰ Sasa, tafadhalini, huu si mzaha. Lakini ilinibidi kumwambia huyo ndugu, nami natumaini lilimsaidia. Si kusema hivyo kuwa tofauti; kama nilifanya hivyo, nilikuwa mnafiki, unaona, nilihitaji kusafishwa, mimi mwenyewe.

Nikasema, “Bwana, ati ulisema mke wako ni mtakatifu?”

Akasema, “Loo, naam.”

²¹¹ Nikasema, “Anaonekana kama ni mtakataka, kwangu.” Nikasema, “Si—sijapata kuona tamasha kama hilo maishani mwangu, kama mke wa mhudumu. Huyu haonekani kama ni mke wa mtu mtakatifu.”

²¹² Na wala kanisa la Mungu aliye hai, likitegemea mitindo yake, karamu zake za chai, na karamu za michezo ya hila, na michezo ya karata, na dansi, na vikundi vya kusogoa, kujipamba namna hiyo, na ulimwengu, kuonekana kama Bibi-arusi wa Mungu Mtakatifu. Wakati anapovuta sigara, na kucheza dansi, na karamu, na mlo wa supu, na kunywa michanganyiko ya vileo vikali, na yote namna hiyo, na kusema hao ni Bibi-arusi wa Kristo? Haonekani kama Mke wa Mtu Mtakatifu, kwangu mimi. La, bwana. Yeye asingechagua kitu kama hicho. Angemchukua mwanamke aliyekuwa sahihi, anayeonekana kama kile alichokuwa akijaribu kuwakilisha. Ninaamini hiyo ni kweli. Hilo huenda likaudhi kidogo.

²¹³ Mama yangu mzee wa kusini ameaga dunia. Nilipokuwa mvulana mdogo, tulikuwa na... Hatukuwa na chakula, hata kidogo, nasi tulikula mbaazi zenye jicho jeusi na ugali wa mahindi. Sijui kama mnajua hivyo ni vitu gani ama hamjui. Kwa hiyo hatukuwa... Hakuwa na mafuta yoyote ya kukaangia mwaka mzima, nasi karibu ilitulazimu kuchukua maskini sufuria kubwa la kale namna *hiyo*, na kuweka ngozi ya nyama ndani yake. Tungeenda mahali wangekata, ama mabucha wangekata nyama na kutupa ngozi. Nasi tungeiyeyusha, tupate mafuta ya kukaangia, na kuyamimina mle.

²¹⁴ Kila Jumamosi usiku, mama alisema tulihitaji dozi ya mafuta ya mbarika. Nami si—siwezi kuvumilia kitu hicho bado. Nami ingenibidi kuyanywa. Ningemjia, nikishikilia pua yangu namna *hii*. Ningesema, “Mama, si—siwezi kabisa kuyanywa.” Nikasema, “Yananichefua sana.”

Kasema, “Yasipokuchefua, hayakufai kitu.”

²¹⁵ Kwa hiyo nafikiri hivyo ndivyo ilivyo na kuhubiri Injili. Kama haikuchochi kidogo, kuchukua ninii yako... kufurahia mlo wako wa kiroho ukianza vizuri, ikuchefue kidogo, upate kujichunguza na Biblia: uone kama hiyo hasira ya kale, na ubinafsi, ukosefu wa utauwa, kuipenda dunia, televisheni, na mambo fulani usiku; na kuacha kanisa likiwa tupu, na viti vikiwa vitupu. Ambapo, unapaswa kuwa huko nje kama Yesu, una Roho Wake ndani yako, ukijaribu kumfanya kila mtu nchini kuja kwenye kanisa lako, kumpokea Kristo. Nasi ati tunajiita basi Bibi-arusi wa Kristo? Loo, ni jambo la kusikitisha jinsi gani, ewe rafiki!

²¹⁶ Saa imewadia. “Bibi-arusi Wake amejifanya tayari.” Loo! “Amejifanya tayari.” Aliweka kando mambo haya yote. Kumbukeni, Esta alichaguliwa, na hao wengine walikataliwa.

Na ni wale tu waliozaliwa mara ya pili, walio na Roho wa Mungu, watakaochaguliwa Siku hiyo, ambaye taji ya utukufu itawekwa juu ya kichwa Chake. Na hao wengine watakataliwa.

²¹⁷ Hebu niwaambie jambo fulani dogo lililotukia. Mimi—mimi, mimi ni mmishenari, kama mjuavyo, ninafanya uinjilisti, kazi ya kimishenari, karibu mara saba nchi za ng'ambo, kote ulimwenguni. Hapa, si muda mrefu uliopita, katika mji wa Rumi, Rumi ni mji mkuu wa sanaa. Nao walikuwa na shule ya sanaa kule, na wengi wa vijana wetu wa Kimarekani huenda huko kila mwaka, kuchukua mafunzo ya mwaka mmoja ama miwili katika sanaa, kujifunza kuchora picha. Kulikuwako na kundi la vijana Wamarekani lililokuja huku, miaka michache iliyopita, kama nilivyosimuliwa hadithi hiyo. Na wanapofika kule, wanaingia tu wazimu wa nguruwe kabisa. Wanapokuwa Rumi, wanafanya kama Rumi ifanyavyo: wanatoka wanaenda kunywa, na kuvua nguo zao, na chochote kile, na kufanya maovu, wavulana kwa wasichana.

²¹⁸ Na kulikuwako na shule fulani. Na katika shule hii, hili—hili kundi la vijana wa Kimarekani lilikuja kule. Na kila mmoja wao, karibu wote, alifanya jambo lile lile. Lakini msichana mmoja mdogo, asingevumilia jambo hilo, hata kidogo. Alibaki ndani. Usiku, yeye alisoma wakati wote walikuwa wametoka kwenda kunywa pombe. Mchana, alifanya kazi, alisoma. Vema, alikuwa mtu wa kuchekwa na shule nzima. Naye alijitunza kama mama wa heshima, akatenda kama mama wa heshima. Ingawa alizungukwa na wavulana wadogo wa Kirumi na kila kitu, wakijaribu kumfanya akatembee, yeye alikataa hilo. La, bwana. Alidumu moja kwa moja na masomo yake, akijifunza jinsi ya kuchora, na kutia rangi, hasa. Naye alidumu nalo.

²¹⁹ Hatimaye, mzee mwangalizi wa mahali hapo aliendelea kumtazama, kwa kuwa aliona alikuwa tofauti sana, ingawa yeye alikuwa Mkatoliki wa Kirumi, aliendelea kumwangelia, jinsi alivyojiheshimu. Jioni moja, msichana huyo mdogo, katika bustani mahali stu—studio hiyo ilipokuwa, mbona, ama mahali ambapo walikuwa na shule hiyo, alitoka kwenye eneo la chuo hicho, na akaelekea kwenye kilele cha kilima, nalo jua lilikuwa likitua. Naye alikuwa amesimama pale juu, akiwa na uso wake mrembo, safi, na nywele zake zikining'inia chini, akiangalia *huko* kuelekea machweo ya jua.

²²⁰ Yule mzee mwangalizi alikuwa akikusanya taka kule chini uani. Aliendelea kumwangelia msichana huyo, wakati akizoa taka. Kitu fulani kiliendelea tu kumwambia, “Nenda, kazungumze naye.” Kwa hiyo akaweka reki yake chini, akavua maskini kofia yake kama tarai, akaenda mahali ambapo yule msichana alipokuwa. Akasafisha koo lake. Msichana akageuka. Akasema, “Samahani, binti.”

Akasema, “Naam, bwana. Hakika.”

²²¹ Naye akaona alikuwa akilia. Hao wengine wote walikuwa wametoka kwenda shamrashamra usiku huo. Akasema, “Binti, natumaini ya kwamba unanielewa kwa njia nzuri, ya kwamba nitazungumza nawe tu.” Kasema, “Umekuwa hapa, kwa karibu muda wa miaka miwili sasa. Nami nimeona kundi ulilokuja nalo, daima wanatoka kwenda kwenye karamu, na wanarudi wakati wote usiku, wamelewa, na nguo nusu uchi, na kila kitu. Lakini nimeona ya kwamba wewe huhudhuri karamu kama hizo.” Kisha kasema, “Ni—nimeona ya kwamba, inaonekana, ya kwamba daima unaangalia ng’ambo ya bahari. Jioni ikifika, unakuja hapa juu, na kusimama hapa kila jioni, na kuangalia jua likishuka.” Kisha kasema, “Ni nini, ni kitu gani kinachosababisha jambo hilo?” Kasema, “Mimi ni mzee. Nami ni—nina hamu ya kujua ni kitu gani kinachosababisha tofauti hii kati yako na hao wengine.”

²²² Akasema, “Naam, bwana.” Akasema, “Bwana, ninaangalia kuelekea nyumbani wakati jua linapotua.” Akasema, “Huko ng’ambo, ng’ambo ya lile jua kule kuna nchi ya uenyeji wangu.” Kisha akasema, “Katika nchi hiyo kuna jimbo fulani. Na katika jimbo hilo fulani kuna mji fulani. Na katika mji huo fulani kuna nyumba fulani. Na katika nyumba hiyo kuna mvulana fulani.” Kasema, “Yeye, pia, ni mwanasanaa. Nilipoondoka, kuja huku, nilimwahidi upendo wangu kwake. Tumechumbiana.”

²²³ Na akasema, “Haidhuru yeyote wa hao wengine anafanya nini, hilo halina uhusiano wowote nami.” Akasema, “Niliahidi kuishi mwaminifu na mkweli.” Kisha akasema, “Ninaitamani ile siku nitakayojisikia nikiwa juu ya mbawa za ile ndege kubwa ambayo itanivusha bahari na kuniweka kwenye uwanja wa ndege ambapo yeye atanilaki. Anajenga nyumba, nasi tutaishi pamoja katika nchi hiyo.”

²²⁴ Ndipo akasema, “Hiyo ndiyo sababu ninatenda jinsi ninavyotenda. Mimi ni mwaminifu kwa ahadi niliyomwahidi mvulana fulani. Naye ni mwaminifu kwa ahadi anayoniahidi.” Kasema, “Ninasikia kutoka kwake, mara kwa mara, nami ninamwandikia, na,” kasema, “tunawasiliana. Tungali tunashikilia nadhiri zetu, tuingojea siku tutakapokutana.”

²²⁵ Loo, jinsi hilo lingefaa kwa Mkristo halisi, kuyaacha mambo ya ulimwengu. Na siku moja, nena kuhusu kuja bandarini, kwenye mbawa za Hua! Yeye anakuja kumchukua Bibi-arusi, yule ambaye hajipumbazi na dunia wala mambo ya dunia. Ameoshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo. Ameweka ahadi ya upendo Wa—Wake Kwake pekee. Kuipenda dunia kumekwisha na kumekufa Kwake. “Arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na Bibi-arusi Wake amejifanya tayari.”

Hebu na tuwazie jambo hilo wakati tukiinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

²²⁶ Siku moja, ninapoangalia kwenye machweo ya jua, mimi pia, miaka thelathini na mmoja iliyopita, nilitoa ahadi kwa Mtu niliyempenda, upendo wangu wote Kwake. Daima nimejaribu kumshikilia Yeye na Neno Lake, kokote niendako. Ninajua kuna wengine wengi wanaoketi hapa ndani, walio wa namna hiyo, wakiingojea ile siku ambapo ile meli ya kale ya Sayuni itakapoingia bandarini, ichukue nafsi zetu na kutupeleka Mbele Zake Yeye tunayempenda na tumemwahidi upendo wetu.

²²⁷ Huenda ikawa kuna wengine hapa ndani usiku wa leo, ambao hawajapata kufanya ahadi hiyo. Huenda ikawa kuna wengine ambao wameitoa na kuivunja. Kama uko katika hali hiyo usiku wa leo, rafiki, mbona usirudi tu usiku wa leo na kufanya upya ahadi yako? Kama hujafanya hivyo, ifanye. Mbona usije ukaifanye usiku wa leo? Useme, “Bwana Yesu, ninakupenda.”

²²⁸ Kumbuka, kama tayari umefanya ahadi yako, na ungali unachanganyana na mambo ya ulimwengu, Yesu hatakuwa na bibi-arusi kama huyo. Hatakuwa na mmoja ambaye ni mzinzi. Upendo wako wote hauna budi kuwa Kwake. Na kama unayapenda mambo ya ulimwengu, na mitindo ya ulimwengu huu, kuliko unavyompenda Mungu, basi hujajifanya tayari.

²²⁹ Je! mtu huyo yupo hapa ndani usiku wa leo, tukiwa tumeviinamisha vichwa vyetu, ungeinua mkono wako, useme, “Ndugu Branham, niombee. Ninataka kuwa hivyo. Ni—ninataka kuwa sehemu ya Bibi-arusi. Nami ninajua ninafanya mambo nisiyopaswa kufanya. Niombee”? Mungu akubariki, dada yangu Mhindi. Mungu akubariki, dada. Na wewe, ndugu yangu. Na wewe, ndugu. Mtu mwingine yeyote? Inua mkono wako, useme, “Niombee, Ndugu Branham. Ni—ni—ni—ninajua mimi siko sahihi.”

²³⁰ Sasa kuwa mwaminifu kwa nafsi yako. Angalia nyuma kwenye maisha yako. Inakubidi kuangalia nyuma kabla hujasonga mbele. Angalia jinsi ambavyo umekuwa. Angalia jinsi ambavyo roho uliye naye amekufanya utende. Kama hujaninii... Kama ukitangaza kwamba wewe ni Mkristo, na bado ungali unachangamana na mambo ya ulimwengu, ndugu, dada, naweza je ila kuwa kipofu kama huoni ya kwamba umekosea?

²³¹ Mtu fulani alisema hivi majuzi, kasema, “Ndugu Branham, inakupasa kuwaacha watu wa namna hiyo.” Kasema, “Watu wanakuita nabii.”

Nikasema, “Mimi si nabii.”

²³² Kasema, “Lakini watu wanafikiri u nabii. Unapaswa kuwa unawafundisha hawa wanawake. Badala ya kuwaambia wawe na nywele ndefu na wavae mavazi mazuri na mambo kama hayo, unapaswa kuwa unawaambia jinsi ya kupata mambo ya kiroho.”

233 Nikasema, “Ninawezaje kuwafundisha aljebra, wakati hata hawatakubali ABC, shule ya chekechea? Hata hawana adabu ya kawaida ya kujisafisha, wakijiita, ‘Bibi-arusi wa Kristo!’” Sisemi hilo kwa hasira. Ninasema hilo kwa upendo wa kiungu.

234 Kama nilivyosema asubuhi ya leo, kama nikikuona ukiteremka mtoni katika mashua, na nione utaanguka kwenye maporomoko, mashua hiyo haitayastahimili, huku mimi nikipaza sauti na nikikupigia kelele, sijaribu kukuudhi. Ninakupenda. Kwa sababu, kama sivyoyai, uhai wako utapotea.

235 Je! kuna mwingine, watakaoinua mikono yao kabla hatujaomba? Ninakuona, huko nyuma. Mungu akubariki, na wewe, wewe. Unajua maisha yako yanaonyesha ya kwamba unakosea. Ungali unaupenda ulimwengu zaidi kuliko kumpenda Mungu, basi kuna kasoro mahali fulani. Jiangalie. Huko kwenye vyumba huko nje, inua mkono wako, useme, “Niombee, Ndugu Branham.” Mungu akubariki. Mungu... Hiyo ni kweli. Kweli kabisa, ni—ninapenda sana uaminifu.

236 Hiyo ndiyo shida ya kanisa la Kipentekoste leo. Hatuna ule uaminifu halisi tuliokuwa nao. Hatuna ujasiri wa ku—kuja na kusema ya kwamba, kukubali tumekosea. Ibilisi amelishikilia kanisa sana mpaka linagaagaa tu katika uchafu wa ulimwengu. Usifanye jambo hilo.

237 Maisha yako mwenyewe yanathibitisha ya kwamba huna kile unachosema unacho. Basi kwa nini usikiri jambo hilo? “Yeye atakayekiri dhambi yake atasamehewa: yeye anayeficha dhambi yake hatafanikiwa.” Huwezi kuificha. Mungu anajua yote kuihusu. Na kama ukiona na unajua ya kwamba huishi sawa, basi kwa nini usikiri jambo hilo, na utoke na ulifanye dhahiri?

238 “Dhambi za watu wengine huwatangulia; wengine zinafuata. Jalia zangu zitangulie. Jalia niseme zangu zote sasa hivi. Acha Mungu azipate vizuri. Hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya.

239 Kumekuwa na kama mikono sita ama minane iliyoinuliwa. Hakika kuna zaidi ya hao katika kanisa hili dogo, usiku wa leo, la watu mia moja ama mia mbili hapa, ama labda mia moja na hamsini. Mungu akubariki, kijana mwanamume. Sasa, Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, dada. Hiyo ni kweli. Mungu akubariki, mwanangu. Hilo ni zuri.

240 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...wanawake wa kipentekoste walikuwa hawakati nywele zao, bali wanafanya hivyo siku hizi. Ni kitu gani kilichotukia? Hawakuwa wakifanya...waki—wakijipodoa. Mama yako hakujipodoa, kama alikuwa mpentekoste. Imekuwaje siku hizi? Kwa sababu wanagaagaa katika mambo ya ulimwengu. Nao ulimwengu unatungalia. Tunadai kuwa Kanisa la utakatifu. Kuna

nini? Hatuonekani kama Bibi-arusi wa Kristo. Kuhusu ninyi wanaume huko nje, jambo lile lile. Ndugu, unatia aibu.

²⁴¹ Baba wa Mbinguni, ninapoangalia upande wa pili, na kufanya wito wa madhabahuni kwa jinsi hiyo, nikiwakemea, nikiwararua, inaonekana kana kwamba ni kali. Lakini ndani yangu ninaumia, wakati ninapojua tunakaribia mwisho. Maskini mashua hizi ndogo zitavunjika, moja ya siku hizi. Mauti yatapiga, na jitihada. Na ni mara ngapi nimeitwa kando yao, na kuwasikia wakisema, “Loo, Ndugu Branham, laiti ningaliyaishi mara nyingine tena.” Basi, wakati hawa wangali wanaweza, Bwana, kulisahihisha!

²⁴² Ninajaribu vizuri niwezavyo. Mungu, jalia Roho Mtakatifu awafunulie watu, ya kwamba ninajaribu tu kuwasaidia, sio kuwakemea. Lakini, kama Paulo alivyosema, wa kale! Mungu, sitaki waudhike, bali ninataka kuwaudhi vya kutosha hata wataona mahali wanakosea.

²⁴³ Ninaomba ya kwamba utawajalia, usiku wa leo, watu hawa, walioinua mikono yao, wakiwa—wakiwa hata na heshima ya kutosha ku—kutambua, mbele za Mungu, ya kwamba wako makosani, nao wanataka kuwa sawa. “Tafuteni, nanyi mtapata. Bisheni, utafunguliwa.” Lakini kama hutabisha kamwe, Yeye atafunguaje? Usipotafuta, utapataje?

²⁴⁴ Jalia Roho Mtakatifu, Bwana, awalete watu hawa wafikie kwenye kujisalimisha kukamilifu kwa Mungu, usiku wa leo. Jalia Baba mkuu wa Bwana wetu Yesu Kristo awatakase, nafsi, mwili, na roho, na awaweke katika Mwili wa Bwana Yesu Kristo. “Kwa maana arusi ya Mwana-Kondoo imekaribia, na Bibi-arusi Wake amejifanya tayari.” Ee Bwana, jalia huu uwe ndio usiku wa maandalizi, kwa kuwa kesho huenda ikawa ndiyo siku tutakayokutana Naye. Hatujui ni saa gani tutakapoitwa kukutana na Yeye. Tujalie, Bwana.

²⁴⁵ Sasa wakati nikiomba, nanyi mmeinamisha vichwa vyenu. Kila mmoja wenu ambaye ameinua mkono wake, kama wewe ni mwaminifu sana kwa jambo hilo, na kweli unalimaanisha, wala huoni haya kuwajulisha watu ya kwamba umekuwa katika makosa! Itakubidi kusimama pamoja nayo huko kwenye ile Hukumu, kwa vyovyote. Na Mungu amekuthibitishia vya kutosha, hata unajua ya kwamba umekosea.

²⁴⁶ Hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa nikihubiri jambo kama hilo. Nilizungumza na kijana mwanamke aliyesimama kule nyuma. Alionekana mwenye hali mbaya sana, binti wa mhudumu. Naye alikutana nami nje ya kanisa, naye alinitusi kwelikweli! Alisema, “Mjinga wee.” Maskini, kipusa, midomo iliyopakwa rangi; nywele fupi, zilizokatwa. Akasema, “Kama nikitaka mtu wa kunizungumzia juu ya jambo hilo, nitampata mtu mwenye akili.” Kasema, “Kamwe usije kwenye mimbara ya baba yangu na kuhubiri kitu kama hicho tena.”

²⁴⁷ Nikasema, “Unataka kuniambia, baba yako, jinsi alivyo mhubiri mzuri na mwaminifu wa Kibaptisti, wala asingehubiri dhidi ya jambo hilo?”

Akasema, “Yeye hakukulipa kuja hapa . . .”

Kasema, “Yeye hakunilipa, hata kidogo. Nilikuja kwa mwaliko.”

Akasema, “Kamwe sitakusamehe kwa jambo hilo.”

²⁴⁸ Nikasema, “Hiyo ni juu yako. Niliifuata tu Injili.” Vichaka vya waridi vilikuwa vikipeperushwa na upepo pale katika upepo huo mdogo. Msichana mrembo.

²⁴⁹ Baadaye kidogo, yapata mwaka mmoja baadaye, nilipitia kwenye mji huo. Nikamwona kijana mwanamke yuyo huyo huku sketi yake inaning’inia chini, akivuta sigara, akitembea barabarani. Nikawazia, “Yule ni mke wa Ndugu *Nanii*, ama, binti.” Nikavuka barabara, nione kama ningeweza kumfikia.

²⁵⁰ Akainua macho yake akaniangalia, akivuta sigara hii, akaipulizia puani mwake. Akasema, “Haloo, mhubiri,” nahau isiyo na kicho, namna hiyo.

Nikasema, “Vema, vema!”

Kasema, “Vuta kidogo sigara yangu. Kuwa mwanamume.”

Nikasema, “Hivi hujionei aibu?”

²⁵¹ Akaingiza mkono akatoa kitabu chake kidogo cha kuandikia cha mfukoni, kasema, “Basi chukua sigara.”

²⁵² Nikasema, “Unatia aibu. Unatia aibu, kumpa mtumishi wa Mungu sigara.”

Akasema, “Basi labda utakunywa pombe kutoka kwenye chupa yangu.”

Nikasema, “Naomba usiseme hivyo.”

²⁵³ Nikamwangalia. Nisingejizua kulia, maana baba yake ni mtu mwema. Nikamwangalia. Nikawazia, “Loo, jamani! Alidhani alikuwa na wakati mwingi sana.”

²⁵⁴ Nikaanza kusonga mbele. Nisingeweza kuyazua machozi kutoka machoni mwangu. Nikasonga mbele. Akasema, “Ngoja kidogo.”

Nikasema, “Naam, mama?”

²⁵⁵ Akarudi nyuma. Ilikuwa karibu ni aibu kuwa nikizungumza naye barabarani, watu wakipitia pale. Akakaribia. Akasema, “Unajua yale uliyoniambia usiku ule?”

Nikasema, “Daima nitakumbuka.”

²⁵⁶ Kasema, “Ninataka kukwambia, mhubiri, ulikuwa unasema kweli.” Akasema, “Nilimhuzunisha Roho Mtakatifu mara ya mwisho.” Sasa, hili hapa tamshi ambalo mwanamke huyo alinitolea, na silisahau kamwe, kadiri niishivyo. Akasema,

“Alikuwa akinishughulikia usiku ule. Lakini,” kasema, “wakati nilipomkataa wakati ule, ulikuwa ndio wangu wa mwisho.” Kasema, “Moyo wangu umekuwa ni mgumu sana; simjali Mungu, kanisa, wala chochote kile. Ninamlaani baba yangu, kila siku.” Halafu akasema, “Ninaweza kuiona nafsi ya mama yangu ikikaangwa kuzimu, kama kitumbua, na kuicheka.” Huko ni kumhuzunisha Roho Mtakatifu kwa mara ya mwisho. Wazia jambo hilo.

²⁵⁷ Hebu na twende Nyumbani juu ya mbawa za Hua. Hebu na tuwe Bibi-arusi. Amka kutoka kwenye kiti chako sasa, kama umekosea. Njoo hapa. Simama hapa madhabahuni na useme, “Nimekuwa makosani. Ndugu Branham, nina hasira. Ama, ni—ni—nimeishi maisha mabaya. Si—sipaswi kufanya mambo haya ninayofanya. Ndugu Branham, nimefanya *hivi, vile*, ama *vinginevyo*. Nina hatia ya kusema uongo. Nina hatia ya kuiba. Nina hatia ya jambo fulani. Sijamtumikia Mungu jinsi ninavyopaswa, nami ninajionea aibu, nami ninataka maisha yangu yawekwe sawa. Hivi hutaniombea hapa usiku wa leo, Ndugu Branham?” Nitafurahia kufanya hivyo.

²⁵⁸ Kama Mungu atayajibu maombi yangu, kuyasikia kwa ajili ya wagonjwa, vipofu, na wanaoteseke, hakika Yeye atasikia maombi kwa ajili ya mwenye dhambi. Hivi hutakuja na kuwa sehemu ya Bibi-arusi usiku wa leo? Ninakualika kuja.

²⁵⁹ Asante, ndugu yangu. Ninafurahia ujasiri wa namna hiyo, utakaotoka nje na kukubali umekosea. Mungu akubariki, ndugu. Simama papa *hapa*.

²⁶⁰ Unataka kuniambia, ungeweza kuinua mkono wako na usiwe mwaminifu juu yake? Ilikuwa je kwa watu? Ndugu, kuna nini? Kuna shida gani na watu wetu siku hizi? Unataka kusema ungeinua mkono wako, ya kwamba ulikuwa umekosea, halafu usije? Na unajua. “Yeye anayejua kufanya mema, wala hayafanyi, kwake ni uovu.” Hivi huwezi kuja?

Wakati mpiga piano, ukiweza, dada, mpiga kinanda, muziki kidogo tu.

²⁶¹ Ninakualika. Ninataka kuwaulizeni. Ni wangapi kwenye kusanyiko hili wamekuwa mkutanoni wakati . . . Mnajua mimi si mhubiri. Sina elimu.

²⁶² Mungu akubariki, msichana. Hilo linahitaji msichana halisi kufanya jambo hilo. Kwaya hii ndogo inayokuja hapa, ubarikiwe, dada yangu. Huo ni ujasiri kwelikweli. Ni—ninapendezwa na maskini msichana huyo. Mungu akubariki, kipenzi. Nina msichana mdogo nyumbani, karibu rika lenu nyote, maskini Rebeka. Ninawathamini. Maskini msichana wa kihindi? Mungu akubariki, kipenzi, maskini binti huyu wa mfalme. Mungu awe pamoja nawe, kipenzi. Wewe, dada mdogo, Mungu awe pamoja nawe. Na wewe, dada.

²⁶³ Sasa, angalieni huku. Kama wasichana wadogo namna hiyo, maskini wasichana wadogo, wenye dhamiri njema; na nimehubiri hotuba inayowakata vipandevipande, nao hawa hapa wanakuja hapa juu, wakijua ya kwamba wamekosea, wanasimama hapa mbele ya umati kutubu. Hakika, hakika ninyi wanawake watu wazima, hivi hamwezi kuja? Songeeni hapa, na msimame upande *huu*.

. . . ningeutafuta uso Wako;
Ponya roho yangu iliyojeruhiwa, iliyo vunjika.

Hebu tuuimbe.

Niokoe kwa neema Yako.
Mwokozi, Mwokozi,
Kisikie. . .

²⁶⁴ Hakika ninyi ni waaminifu vya kutosha kuomba maombi manyenyekevu. “Niite, Bwana, nijaribu, na uone kama kuna jambo lolote baya nami.”

Usinipite.

Mungu akubariki, dada mpendwa.

²⁶⁵ Ni wangapi katika mkutano huu wamesimama na kuona, katika kusanyiko, wanawake, wanaume, na wote, wakija wakati nilipokuwa nimesimama nikiwaombea wagonjwa, na Roho Mtakatifu anawaambia mambo, juu ya dhambi zao na kadhalika, na wanajua? Ni wangapi wenu wanaojua hiyo ni kweli? Kamwe hashindwi. Roho Mtakatifu ananiambia, Roho Mtakatifu yeye huyo, kwamba kuna kitu fulani hapa ndani usiku wa leo kinachomhuzunisha. Sasa, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Sasa, kabiliana nacho hapa, ama Kule.

²⁶⁶ Mimi si mtu anayeshikwa na mihemuko. La, bwana. Ninajua kabisa ninaposimama, na ni—ninamjua Mungu. Hiyo ni kweli. Kuna wengi wenu mnaopaswa kuwa mmesimama papa hapa ambapo wasichana hawa wadogo walipo. Sasa, hivi hamwezi kuja? Ninawaalika. Sitawabembeleza. Ninawaambia tu.

²⁶⁷ Mtu fulani alisema, “Sijapata kusikia wito wa madhabahuni ambapo mhudumu alilikemea kusanyiko, katika mambo kama hayo.”

²⁶⁸ Hivyo ndivyo inavyopaswa kufanywa. Huji huku kwa hadithi ya kuhuzunisha, mama fulani akifa ama chochote kile. Hilo, hilo liko kwenye mhemuko. Unakuja kwa Neno la Mungu. Huji chini ya mhemuko wowote. Unakuja ukiamini ya kwamba Mungu ni Mungu, nawe uko katika nyumba ya hukumu ya Bwana. Nawe unakuja, ukisihi kwa ajili ya kesi yako.

²⁶⁹ Mungu akubariki, ndugu yangu, dada yangu. Ninataka kukupa mkono, niseme ninathamini imani yako nyofu. Msichana mdogo, ninakuthamini. Mungu akubariki. Na akupe Roho hiyo hodari. Ubarikiwe, ndugu yangu. Mungu awe pamoja nawe.

270 Mara nyingine tena, ndipo tutafunga. Huenda ukafungwa kwa mara ya mwisho, pia. Unaona? Sijui ni lini. Natumaini hautafungwa. Lakini huenda ukafunga. Unaona?

Mwokozi . . .

271 Njoo hapa, dada yangu. Ninataka kukupa mkono, asante. Ninathamini imani hiyo. Hiyo ni imani halisi.

272 Njoo hapa, ndugu yangu. Ninataka kukupa mkono, papa hapa. Ninathamini uaminifu wako. Mungu akubariki.

273 Njoo hapa. Mungu akubariki. Ninathamini uaminifu wako, kuchukua msimamo kwa . . .

. . .-sinipite.

Mwokozi . . .

274 Ati nini? “Arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na Bibi-arusi Wake amejifanya tayari.”

. . .kilio changu kinyenyekevu

Unapopita . . .

Usinipite.

Ati nini?

Nikitegemea haki Yako pekee,

Nitautafuta uso Wako,

Ponya moyo wangu uliojeruhiwa, na kuvunjika

(Mahali ambapo Neno lilikata na kuingia),

Niokoe kwa neema Yako.

Mwokozi, Mwokozi,

Sikia ninii yangu nyenyekevu . . .

Unapowaita wengine,

Loo, usinipite.

275 Kumbuka, Roho Mtakatifu ndiye aliyeupenya moyo wako, ukaja hapa. Wazia tu mahali alipokata, na mtu huyo kamwe hataishi chini hivyo. Daima watakumbuka jambo hilo. “Mioyo yetu isipotuhukumu.” Lakini unapokuja na kitu fulani katika Neno la Mungu, na kukwepa jambo hilo, huyo si Uzao wa Ibrahimu. Ibrahimu alishikilia ahadi ya Mungu moyoni mwake, haidhuru hali ilikuwaje.

276 Ninawathamini hawa wote wanaosimama kuyazunguka madhabahu. Maombi yangu kwenu, ya kwamba Mungu atawapa shauku ya moyo wenu usiku wa leo, na kuwafanya watu watakatifu halisi.

277 Baadhi ya hawa vijana wadogo, hawa hapa ni Wahindi, Wahispaniola, Wameksiko, wote wamesimama hapa, watu ambao wamedai kuwa ni Wakristo, labda, kwa miaka kadhaa, lakini wameona ni makosa. Wanataka kuwa sawa. “Heri walio na njaa na kiu ya haki, kwa maana watajazwa.” Wamehukumiwa, wako tayari kujiweka sawa na Mungu, kupitia kwenye madhabahu inayowaka moto ya hukumu ya Mungu.

278 Inabidi kukabiliana nalo mahali fulani, marafiki. Huna budi kukabiliana nalo mahali fulani, kwa hiyo kabiliana nalo hapa. Usingojee hadi asubuhi. Unaweza ukauawa usiku wa leo, katika ajali, ukienda nyumbani.

279 Hivi majuzi tu katika mkutano fulani, nilifanya wito wa madhabahuni, na—nami nikaita, kama ilivyokuwa huko Ohio. Na usiku huo, niliondoka jengoni, na nilikuwa nimeondoka yapata dakika kumi na tano. Nilimsikia mtu fulani akipiga mayowe, kando ya barabara. Nikasimama, nikaenda kule. Gari moja lilikuwa limepata ajali, limegongana na lingine. Na mwanamke aliyeketi pale, akiwa na wasiwasi sana, alitoa pete yake, alikuwa na wasiwasi sana. Aliuawa. Naye alikuwa akizungumza na binti yake, akishuka kwenda barabarani, ambapo alikuwa akiendesha. Walimweka pale, akiwa tayari kupelekwa hospitalini. Na wote wawili walipaswa kuja madhabahuni. Naye huyo binti akasema, “Mama, neno la mwisho aliloniambia kabla gari halijagongana, ‘Nilifanya kosa usiku wa leo. Ninajua nilifanya kosa.’” Na hapo uhai wake uliitwa.

Loo, unasema, “Hilo halitanipata mimi.” Huenda likakupata. Huenda likakupata.

280 Na vipi kama Roho Mtakatifu asipokuhukumu tena na kukwambia umekosea? Basi uingia katika Umilele namna hiyo. Nawe unajua, ukiwa na roho wa namna hiyo, huwezi kufanya hivyo. Bwana, angalia nyuma kote katika maisha yako, angalia jinsi ulivyoishi. Kisha uangalie huko nyuma uone kama ni maisha hayo ya upendo, manyenyekevu ya Kristo, yakilingana na Neno Lake lote. Yasipolingana, basi njoo uwe sawa. Kuna . . . Kwa nini, kwa nini uchukue kabadala, wakati mbingu zimejaa baraka halisi za kipentekoste ambazo zitausafisha moyo wako, zitaitikasa nafsi yako? Hiyo si ni kweli?

281 Ni wahudumu wangapi waliomo humu ndani usiku wa leo? Ninataka baadhi yenu ndugu mtoke mje hapa pamoja nasi. Hilo ni sawa, ndugu? Naam. Njoni hapa juu, sivyo, kwa dakika moja, ndugu? Hiyo ni kweli.

282 Yesu alisema, katika Neno Lake, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele; hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Yohana Mtakatifu 6 ilisema, “Nami nitamfufua tena katika siku ya mwisho,” ufufuo.

283 Enyi watu, sisi, inatubidi kustahimili jambo hilo. Hatuna budi kufanya jambo hilo. Haina budi tu kufanywa. Kwa hiyo ninii . . . Si mhemuko. Mihemuko inaambatana nalo, hakika. Hilo ni kweli. Lakini jambo ni kwamba, ni moyo uliowekwa wakfu.

284 Lichukue tu Neno la Mungu, na useme, “Mungu, nilifanya makosa. Ninasikitika nilifanya jambo hilo. Unajua moyo

wangu. Nilifanya makosa. Papa hapa mahali hapa, ninakiri makosa yangu. Na tangu usiku huu, kuendelea, mimi nimeposwa na Wewe. Mimi ni sehemu ya Bibi-arusi. Sitafanya jambo *hilo* tena; kamwe usiache hasira yangu ipande tena. Nitaninii—nitatenda kama mama wa heshima. Nitatenda kama muungwana. Nitafanya mambo ambayo Biblia inasema yafanywe. Nitakuchukua kwenye Neno Lako moja kwa moja sasa hivi.” Basi unafikia mahali fulani.

²⁸⁵ Mnaamini jambo hilo, enyi wahubiri wa Injili? [Wahudumu wanasema, “Amina.”—Mh.] Hilo ni Kweli? [“Amina.”] Hiyo ni kweli.

²⁸⁶ Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu katika maombi sasa, kila mmoja wenu, katika njia yako mwenyewe.

²⁸⁷ Kumbukeni, moja kwa moja karibu nanyi ni Kristo. Mbele yenu, hapa madhabahuni, wamesimama Wakristo wakiomba. Nyuma yenu; wahudumu wa Injili wanaomba. Sasa, hilo linakuweka katika mazingira ya maombi.

²⁸⁸ Sasa, maungamo yenu, mioyoni mwenu, katika njia yako mwenyewe. “Bwana, nimekosea.” [Hao walio madhabahuni wanasema, “Bwana, nimekosea.”—Mh.] “Ninasikitika, Bwana,” [“Ninasikitika, Bwana,”] “Nilifanya mambo haya.” [“Nilifanya mambo haya.”] “Sasa ninaungama dhambi yangu.” [“Sasa ninaungama dhambi yangu.”] “Ninakuamini Wewe.” [“Ninakuamini Wewe.”] “Ninakukubali Wewe sasa.” [“Ninakukubali Wewe sasa.”] “Ninataka kuwa sehemu ya Bibi-arusi.” [“Ninataka kuwa sehemu ya Bibi-arusi.”] “Katika Jina la Yesu ninaomba.” [“Katika Jina la Yesu ninaomba.”] Sasa, weka maungamo yako moyoni mwako sasa.

Sasa nitawaombea.

²⁸⁹ Baba wa Mbinguni, jinsi inavyonihuzunisha wakati mwingine ninapowaangalia watu wanaonipenda, na kuona jinsi ambavyo Wewe unalichukua Neno na kuliweka pale. Linakata tu hadi mafuta ya mfupa, lakini basi unakuja moja kwa moja na kulithibitisha kwamba ni Kweli. Ni Kweli.

²⁹⁰ Hawa hapa wanaume na wanawake wamesimama, hata wasichana wadogo, wasichana wadogo wamesimama hapa wameinamisha vichwa, na machozi machoni mwao, moja kwa moja kwenye njia panda za maisha. Ninafikiria mahali ambapo wangeishia, kule chini katika kundi lile la roki, ya kukata viuno, lililopagawa na pepo, linaloteswa na pepo. Hawa hapa, wamesimama hapa usiku wa leo wakiwa wameinamisha mioyo, wakitaka kitu fulani wanachoweza kukishika kwa mikono yao, kusema, “Bwana Mungu, nisafishe na vitu vyote vya ulimwengu.”

²⁹¹ Hawa hapa wanaume wa umri wa makamu, vijana wanaume, wanawake wazee, wasichana, wote wamesimama pamoja. Wanakiri kuna kosa. Ulisema na moyo wao; kamwe wasingeweza

kuwa hapa. Inaonyesha ya kwamba hata wasingeweza kuinuka kutoka vitini mwao, bila ya kuwako na uamuzi uliofanywa tayari. Roho wa Mungu alikuwa karibu nao, na—na akasema, “Umekosea.”

Nao maskini uhai wao ukasema, “Bwana, basi ninakutaka Wewe.”

Naye ibilisi akasema, “Tulia.”

²⁹² Lakini Roho wa Mungu alisema, “Simama.” Nao wametembea katika utiifu, na kusimama hapa madhabahuni.

²⁹³ Sasa, kama vile ambavyo nimekunukulia Neno Lako, “Yeye ajaye Kwangu, sitamtupa nje kamwe. Hata dhambi zako zikiwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; nyekundu kama damu, nyeupe kama sufu. Njoo mnunue Kwangu, divai na mafuta. Neema yangu yatosha. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele; wala hataingia Hukumuni, bali amepita toka mautini kuingia Uzimani. Na sasa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na Bibi-arusi amejifanya tayari.”

²⁹⁴ Baba, wao ni Wako. Wao ni nyara za Neno Lako. Wapo hapa wapate kuoshwa kwa maji ya Neno, kwa sababu ni Injili kamili. Haiachi chochote. Imekata, kufikia kwenye shule ya chekechea. Inang’oa mizizi, mizizi ya uchungu, mi—mi—mizizi ya kutojali, mizizi ya ulimwengu. Ing’oe, Bwana, kwa Roho Mtakatifu. Itupe mbali na watu hawa.

²⁹⁵ Ninawadai kwa ajili Yako usiku wa leo, Yesu, kama hazina Yako mwenyewe, kama vito katika taji Yako, kama washiriki wa Bibi-arusi Wako. Ninayadai maisha yao. Ninaomba kwa moyo wangu wote, pamoja na wahudumu hawa, watumishi hawa wa Mungu aliye hai. Ninaomba ya kwamba utawaondolea, Bwana, mambo ya ulimwengu, na kuwapa ujasiri wa kusimama mbele ya Shetani. Tujalie, Bwana. Tunaamini ya kwamba utafanya jambo hilo. Wewe ulisema, “Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya.” Sasa, kamwe hukusema, “A-ha, labda nitaifanya jambo hilo.” Ulisema, “Nitalifanya.” Nami ninaamini hiyo ni kweli.

²⁹⁶ Sasa, pia imeandikwa katika Maandiko, “Katika Jina Langu watatoa pepo.” Ibilisi ndiye ambaye angemchukua msichana mdogo ama mwanamke, na kuyaangamiza maisha yake. Ibilisi ndiye angemchukua mwanamume na kuyaangamiza maisha yake. Nami nitanukuu hadithi hii ndogo, Bwana, katika maombi yangu. Nami ninaomba ya kwamba Wewe utanisikia, na utayajibu maombi yangu, ya kwamba kila mmoja wa hawa atadaiwa usiku wa leo kwa ajili ya vito vya Ufalme. Wao wamekuja. Nami sina budi kuwajibika kwa ajili ya maneno yangu usiku wa leo. Na hawa hapa wamekuja kusimama pamoja nami, na kuchukua mahali petu karibu na Kristo.

²⁹⁷ Sasa, Shetani, umeshindwa. Uliwazuia wachache wao, bali hukushinda vita. Yesu alisema, “Yeye anijiaye Mimi, sitamtupa kamwe.”

²⁹⁸ Shetani, nakwambia, ya kwamba siku moja kulikuwako na mvulana mdogo aliyekuwa akiwachunga kondoo wa baba yake. Na simba akaingia na kumchukua mmoja wao, akamtoa nje, akamtendea maovu, na alikuwa akienda kumla. Lakini huyu mchungaji mdogo wa kweli, hakuwa na mengi ila kombeo, bali alikuwa na imani katika Mungu aliye hai. Alimfuatilia huyo simba, naye akamshika, na aka—akamwua. Alimshambulia, naye akamshika ndevu na kumwua. Akamtoa huyo kondoo mdomoni mwake, akamrudisha malishoni kwa uponyaji wake.

²⁹⁹ Umewachukua kondoo hawa wa thamani wa Mungu, mama hawa, ambao uliwafanya wakate nywele zao na kujipodoa, na kuonekana kama mambo ambayo Biblia inayakemea, nawe ulifikiri uliwapata. Lakini ninakuja na kombeo hili dogo rahisi la maombi. Ninawarudisha usiku wa leo. Huwezi kuwashikilia zaidi. Umeshindwa vita. Hawa wanaume wa thamani wanaosimama hapa, wana-kondoo wa Mungu, waachilie. Tunakuapiza, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Ninaweka kati ya tabia hizi na hasira, na matendo mabaya na chochote kile, ninaweka Damu ya Yesu Kristo, kwa imani, kati yao na kitu hicho tena. Hutawashika tena. Wako malishoni mwa Baba. Wao ni watoto Wake. Ondoka kwao. Katika Jina la Yesu Kristo, ninakuapiza.

³⁰⁰ Hakuna ibilisi kuzimu anayeweza kuwagusa ninyi, kama mtaamini jambo hilo. Mmefunikwa na Damu. Mmazingirwa na maombi, wahudumu wa Injili, na wajumbe wa agano, maombi. Kila mmoja wenu anayesimama hapa, ulikuja hapa, ukijua ya kwamba ulikuwa na tabia, makosa, na mambo ambayo uliyaonea aibu. Kama sasa ukiyaweka kwenye madhabahu ya Mungu ya shaba ya hukumu, na utalikubali sasa kama msamaha wako, kwamba Kristo anakupa, je! utajitolea kwa imani, kuinua mkono wako na kusema, “Sasa nakubali jambo hilo. Limekwisha. Na tangu leo na kuendelea, sitalifanya tena”? Umeokolewa kwa Damu ya Yesu Kristo. Amina. Amina. Mungu asifiwe.

Kuna mwingine yeyote angetaka kuja, kujiunga na kundi hili?

³⁰¹ Je! kuna mgonjwa yeyote humu jengoni, angetaka kusimama kwa ajili ya maombi kwenye wakati uu huu? Simama.

³⁰² Ninataka kila mmoja wenu hapa, kama wewe si ninii—kama wewe si mshiriki wa kanisa fulani zuri la Injili yote, uende kwa mojawapo, hili kama ukiweza, kama unaishi hapa karibu. Kutana na mchungaji na ukabatizwe. Halafu basi kama hujampokea Roho Mtakatifu, mwombe Mungu akupe Roho Mtakatifu na kukujaza, akufanye mshiriki wa Bibi-arusi.

³⁰³ Angalieni huko kote, ndugu, kwa hao wagonjwa. Ibilisi hawezi kuwashikilia watu hao. Huu ni wakati wa kuachiliwa. Haleluya! Hivi hamwamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Hebu basi na tuinamishe vichwa vyetu kwa ajili ya maombi.

³⁰⁴ Na kila mmoja wenu ninyi watu huko nje, walio wagonjwa, ninyi mnaosimama, wekeaneni mikono mmoja kwa mwingine. Yesu Kristo alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Wekeaneni mikono mmoja kwa mwingine. Sasa, usijiombee mwenyewe. Wewe mwombee mtu mwingine uliyemwekea mikono, maana wanakuombea.

Hebu na tuombe pamoja sasa kama Kanisa la Kikristo.

³⁰⁵ Bwana Yesu, tunashukuru kwa ajili ya ushindi usiku wa leo, nafsi zikikujia Wewe. Sasa, ibilisi amewachukua baadhi ya kondoo Wako, kwa wagonjwa. Tunakuja kuwadaa warudishwe. Na kama Kanisa la Mungu aliye hai, tunamkemea ibilisi, na kusema, “Waachilie watu hawa wagonjwa, Shetani. Tunakuapiza katika Jina la Yesu Kristo, kwamba wapate kuponywa.” Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Hiyo ni ahadi ya Mungu, nasi tunajua ya kwamba ni kweli. Wameponywa kwa mapigo ya Bwana Yesu Kristo.

³⁰⁶ Sasa, kama mnaamini jambo hilo, inueni mikono yenu na kumtukuza Yeye. Amina.

³⁰⁷ Vema, mchungaji, yote ni yako. Mungu akubariki, ndugu. Inapendeza sana kuwa pamoja nawe usiku wa leo. Mungu awe pamoja nawe.

Mungu awabariki, enyi ndugu hapa.



ARUSI YA MWANA-KONDOO SWA62-0121E
(The Marriage Of The Lamb)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 21 Januari, 1962, katika Maskani ya Ushirika huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org